Nipashe
Jumanne Julai 16, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581739
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 21



**YAMAL AVUNJA REKODI YA PELE HISPANIA IKIBEBA EURO**

UKURASA 4

**Ajali** ilivyoua wawili, kujeruhi 16 Songwe

UKURASA 5

**TASAF** kuondoa 400,000 kundi umaskini uliokithiri



UKURASA 5

**Mwisho** wa matumizi mita Luku za zamani Novemba

# Mchechu: Mabasi ya mwendokasi kuja kivingine

• **100** kuwasili nchini wakati wowote... *Endelea ukurasa 2*



Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Marekani kuachia fedha za FBME ilizozishikilia miaka 9

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 19

### KAGAME ATABIRIWA USHINDI RWANDA



WACHAMBUZI wa masuala ya kisiasa nchini Rwanda wametabiri ushindi wa Rais Paul Kagame kutokana...

UKURASA WA 20

### GAMONDI AJIFUNGIA KUISOMA VITAL'O KUELEKEA MECHI CAF

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amesema siku mbili tatu zijazo ataanza kazi ya kuichunguza timu ya Vital'O ya Burundi ambayo watacheza nayo katika mechi ya ...



## Rais Samia aomba muda kushughulikia ugawaji wilaya

UKURASA 3

**MICHEZO** **SAMIA/KATAMBI CUP YAZINDULIWA SHINYANGA** UK.20

**MAONI,** UK.6




Balozi wa Marekani nchini, Dk. Michael Battle (wa pili kushoto) akiwa pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa AHEAD Inc, Dk. Donna Williams Ngirwa (kushoto), Mkurugenzi Msaidizi, Wizara ya Afya, Dk. Ahmad Mohamed (wa tatu kushoto) na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu Msaidizi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Winnie Mpanju Shumbusho, wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Afya 2024 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. .PICHA:MPIGAPICHA WETU

# Mchechu: Mabasi mwendokasi kuja kivingine

**Na Gwamaka Alipipi**

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu ameainisha mikakati mitatu ya kufufua Usafiri wa Mabasi yaendayo Haraka (BRT), maarufu 'mwendokasi', ikiwamo uagizaji wa mabasi 100 yatakayowasili muda wowote.

Amesema usafiri huo kwa sasa ni 'uchafu wa moyo' kwa Watanzania na serikali imeshaweka mikakati imara ya kuhakikisha unakuwa mkombozi.

Alikuwa akizungumza na wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wake uliolenga kuelezea mkutano wa 'CEO Forum 2024' unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi ujao jijini Arusha.

"Hayo mabasi yakija yatajikita katika njia kuu kwanza na sio zile njia za mrisho. Lengo ni kuhakikisha tunaondoa shida zote za usafiri katika mradi huo," alihakikisha Mchechu.

Alitaja mkakati wa pili ni kukaribisha wawekezaji wengine watakaoweza kuhudumia mradi huo ambao hawatapungua wanne.

Mchechu alisema hatua ya kuweka wawekezaji wengine itarahisisha utoaji huduma, pia itasaidia kufahamu mtoa huduma gani anatoa huduma nzuri.

Mkakati wa tatu ni kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato, ambao utasimamiwa na kuboreshwa na Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka (Dart).

"Hadi kufikia Agosti, mwaka huu watakuwa wameshakamilisha mchakato wa kusimika mifumo hiyo ya ukusanyaji mapato. Lengo ni kuondoa wizi," alisema Mchechu.

Aidha, alifafanua kuwa matatizo yaliyopo sasa katika mradi huo yalisababishwa na uwekezaji uliofanyika miaka ya nyuma ambao ulikuwa unahudumiwa na sekta binafsi, huku serikali ikiwa na hisa kidogo.

Kwa sasa serikali inamiliki hisa za asilimia 85 na kuna mikakati imewekwa ya kuhakikisha mradi huo unakuwa fahari kwa Watanzania.

"Tunaona changamoto inayotokea kwasasa kwenye usafiri wa mwendokasi na tunajua namna inavyochafua taswira ya mwendokasi nchini, kwa sasa serikali ina umiliki mkubwa kwenye kampuni ya Udart, hivyo tayari tumeanza mpango wa kutatua changamoto zinazojitokeza kwenye usafiri huu tukishiriakiana na taasisi za fedha ikiwamo benki," alisema Mchechu.

Mradi wa BRT umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu hali inayolalamikiwa na wananchi wengi wanaotumia kwenda katika shughuli zao.

Baadhi ya malalamiko ni uchache wa mabasi, msongamano wa abiria vituoni kwa kupoteza muda mwingi kusubiri gari.

Pia, nyakati za mvua mradi huo umekuwa ukisimama kutoa huduma kutokana na sehemu ya Jangwani ambayo imepitiwa na miundombinu ya mradi huo kufurika maji.

**MKUTANO**

Kuhusu mkutano wa CEO Forum 2024, Mchechu alisema utawakutanisha wenyeviti wa bodi na watendaji wakuu kutoka taasisi na mashirika ya umma 253.

Alisema wakuu hao watajadiliana, kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo muhimu ya kuimarisha utendaji kazi na usimamizi wa taasisi ili kuleta tija na ufanisi uliokusudiwa.

Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan na kaulimbiu itakuwa ni 'Mikakati ya taasisi na mashirika ya umma kuwekeza nje ya Tanzania'.

Maeneo muhimu yatakayofanyiwa kazi katika mkutano huo ni kujadili hatua zilizotakiwa katika utekelezaji wa maazimio yaliyokuwa katika kikao kazi cha mwaka 2023.

Pia kujadili fursa za kikanda na kimataifa kwa ajili ya taasisi na mashirika kuwekeza nje ya nchi, kupata uzoefu wa kiutendaji kutoka kwa wataalamu wa ndani na nje ya nchi waliofanikiwa kiutendaji mfano nchi ya Singapore, China, UAE na Afrika Kusini.

Alisema pia watajadili namna bora ya kuboresha mitaji ya mashirika ili kuleta ufanisi wa kiutendaji na kuongeza ushindani.

"Tutabadilisha mitazamo na kuzifanya taasisi na mashirika yetu kuwa vichocheo vya maendeleo ya kiuchumi; Tutapitia kwa pamoja na kukumbushana kuhusu mambo mengine muhimu ambayo wenyeviti wa bodi na watendaji wakuu wanapaswa kuzingatia katika usimamizi wa utendaji kazi," alisema Mchechu.

Changamoto mbalimbali za kiuendeshaji katika taasisi pamoja na kuainisha mikakati ya kukabiliana nazo.

Alisema matokeo yanayotarajiwa baada ya kufanyika kwa mkutano huo ni pamoja na taasisi kujielekeza katika uwekezaji wa nje ya nchi.

Alisema lingine ni kuona taasisi zikiendeshwa kwa ufanisi, zile zinazofanya biashara zitaongeza faida na hivyo kutoa gawio kwa mujibu wa sheria.

Tarajio lingine ni taasisi ambazo zilianzishwa kwa misingi ya kutoa huduma zitaongeza uwezo wa kujitegemea katika uendeshaji na kuendelea kuwapo kwa mfumo endelevu wa kuzitambua taasisi zinazofanya vizuri na kuchukua hatua stahiki kwa taasisi ambazo hazifanyi vizuri.

**WENYEVITI WA BODI**

Aliwaagiza wenyeviti wa mashirika ya umma na taasisi kuwa na mpango mkakati wa kuandaa viongozi wapya wa mashirika ili kuleta ufanisi na utendaji.

"Muwe mnaandaa viongozi wawili au watatu ili inapotokea Mkurugenzi ameondolewa au amestaafu kunakuwapo na mwingine wa kuendeleza shirika ambaye ni mzoefu, sio anakuja mtu mwingine nje ya shirika ambaye anaanza moja kujifunza. Hii inadidimiza ufanisi," alisema.

**TAASISI KUPUNGUZWA**

Taasisi au mashirika ya umma ambayo hayana umuhimu yataondolewa na zingine kuungwanishwa, lengo ni kuwa na taasisi chache zenye faida na mchango kwa taifa.

"Rais Samia amekuja na falsafa ya R4 ambazo ni Reconciliation, Resilience, Reforms & Rebuilding. Katika utekelezaji. Hivyo sisi tumechukua R2 yaani Reforms & Rebuilding katika safari yetu ili kuleta mabadiliko ya mashirika pamoja na yachangie katika uzalishaji nchini," alisema Mchechu.

**UTOAJI GAWIO**

Lengo la ofisi ya Msajili wa Hazina ni kuhakikisha mapato yasiyo ya kikodi yanazalishwa na mashirika ya umma pamoja na taasisi.

Alisema ofisi ya Msajili wa Hazina inakwenda kupitia bajeti za mashirika ya umma pamoja na mapato, lengo likiwa ni kuangalia endapo kinachotolewa ndicho kinachozalishwa.

**MIKATABA**

Kadhalika, alisema wanakwenda kupitia mikataba ya uendeshaji wa taasisi ambayo serikali ina umiliki wa hisa kadhaa, akitoa mfano kwa kuanza wameshapitia katika kampuni 10 za uchimbaji madini ambayo serikali ina umiliki wa hisa asilimia 16.

# Marekani kuachia fedha za FBME ilizozishikilia miaka 9

**Na Grace Gurisha**

SERIKALI ya Marekani imeahidi hadi Desemba, mwaka huu, itaachia fedha zinazomilikiwa na benki ya FBME Ltd inazozishikilia na wadai wote watalipwa ikiwamo Kampuni ya Coast Textile Limited, ambayo inadai Sh. bilioni 145 kulingana na amri ya mahakama iliyotolewa miaka tisa iliyopita.

Wakili wa Serikali Edwin Wediro, alidai katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana kuwa Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Isaack Kihwili, amewasiliana na Ubalozi wa Marekani kuhusu uwezekano wa kuondoa zuio la kushikilia fedha hizo.

"Taarifa nilizonazo ni kwamba amri ya kushikilia fedha hizo itaondolewa na Serikali ya Marekani ifikapo mwisho wa mwaka huu na wadai wote watalipwa," Wakili wa Serikali alidai mbele ya Jaji Salma Maghimbi, wakati shauri la utekelezaji wa hukumu ya mahakama kuhusu fedha hizo lilipokuja kwa ajili ya kutajwa.

Aidha, alidai kuwa Mkurugenzi wa DIB na Mfilisi wa Benki ya FBME nchini Cyprus, walifanya kikao mwezi uliopita, kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na maendeleo ya mchakato wa ufilisi.

Wakili wa Serikali alidai mahakamani kuwa kundi jingine la wateja walioweka amana kwenye benki hiyo katika asilimia 70 ya madai iliyobaki, litalipwa ifikapo Septemba, mwaka huu. Hata hivyo, alidai kuwa Kampuni ya Coast Textile Ltd haitakuwa miongoni mwa wanufaika katika orodha ya mwezi Septemba.

Aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa kusubiri matokeo ya uamuzi wa mamlaka nchini Marekani kuondoa zuio la fedha za Benki ya FBME, ambazo zinashikiliwa kwa tuhuma za kuhusika na madai ya utakatishaji fedha.

Kabla ya kuahirishwa kwa shauri hilo, Wakili Joseph Rutabingwa, anayeiwakilisha Kampuni ya Coast aliikumbushia mahakama ilichomwagiza Mkurugenzi wa DIB kuwasiliana na Serikali ya Marekani kuhusu kuwapo kwa hukumu za mahakama dhidi ya Benki ya FBME, ambazo ni nne.

Jaji Maghimbi aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba Mosi, 2024 kwa ajili ya kusikilizwa.

Katika kesi hiyo, Kampuni ya Coast Textiles Limited iliamua kuomba mahakama kuingilia kati baada ya FBME, ambayo shughuli zake zilichukuliwa na BoT, kushindwa kutekeleza hukumu iliyotolewa na Jaji Aloysius Mujulizi, mwaka 2015 kuhusu malipo hayo.

Kampuni ilifungua maombi ya kukazia hukumu hiyo, ikiomba jumla ya Sh. bilioni 145.94 ipatikane kutoka kwa DIB, wafilisi wa FBME, na Mkurugenzi wa Bodi akishindwa kulipa atalazimika kuwajibishwa.

Mei 20, 2022, Jaji Amir Mruma, aliamuru Mkurugenzi wa DIB, ambaye aliteuliwa na BoT kama mfilisi wa FBME, kulipa kiasi hicho baada ya kukubali maombi ya utekelezaji wa hukumu yaliyowasilishwa na Coast Textiles Limited.

## HABARI KITAIFA

# Rais Samia aomba muda kushughulikia ugawaji wilaya

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameomba apewe muda wa kushughulikia maombi ya ugawaji wa wilaya kutokana na utekelezaji kuhitaji fedha.

Aidha, aliahidi kutoa Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya kununua eneo la kujenga mabweni ya wanafunzi wa Chuo cha Kilimo cha Sokoine, Kampasi ya Mizengo Pinda kilichoko katika mkoa huo.

Rais aliyasema hayo jana katika eneo la Kibaoni, Wilaya ya Mpimbwe, Mkoa wa Katavi, wakati akijibu maombi ya Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda.

Akijibu maombi hayo, Rais Samia aliomba apewe muda wa kulifanyia kazi suala la kuanzisha wilaya nyingine katika mkoa huo kwa kuwa ni gharama kutokana na kuhitaji utawala mpya.

"Tuachieni kidogo tufanye kazi kwa sababu maombi ya kukata wilaya mpya yapo mengi sana, kwa hiyo tunayafanyia kazi kulingana na uchumi unavyokuwa na jinsi mnavyozalisha, tukiuza na kupata zaidi," alisema.

Aidha, Rais aliahidi kutoa Sh. bilioni 1.6 alizoomba Waziri Mkuu mstaafu Pinda kwa kwa ajili ya kulipa fidia wananchi watakaotoa maeneo ya ujenzi wa mabweni la chuo ili kuwaondolea usumbufu wa malazi wanafunzi wa chuo hicho.

Alisema pia alipokea maombi ya kutangaza Hifadhi ya Taifa ya Katavi katika filamu ya Royal Tour na kumwagiza ajipange na akiwa tayari atakwenda kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Alizishukuru kamati za ulinzi na usalama za mkoa na wilaya, viongozi wa dini, vikundi vya sanaa pamoja na waandishi wa habari walioikuwa naye tangu mwanzo wa ziara hiyo.

Akitoa maombi hayo kwa Rais Samia, Pinda alisema ujenzi wa mabweni hayo utasaidia wanafunzi katika chuo hicho kupata eneo la uhakika la kuishi wakati wa masomo.

Alisema eneo hilo kwa sasa ni dogo na anaomba apatiwe kiasi hicho cha fedha ili wanunue maeneo kutoka kwa wanakijiji kwa ajili ya kujenga mabweni hayo.

"Kwa hiyo tunafarijika kwamba mkoa huu ambao ni wa kilimo unapata bahati ya kuwa na kitengo muhimu sana katika mfumo wa utoaji wa elimu," alisema.

Aidha, alimwomba Rais wanapofanya matangazo ya vivutio vya utalii maarufu kama Royal Tour awamu ya pili, watembelee na mkoa huo ili waitangaze Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

Alisema hifadhi hiyo imejaaliwa vivutio vya kipekee ikiwamo uoto wa asili mzuri na wanyama kama vile tembo na twiga wenye ukubwa tofauti na wengine wa aina hiyo hivyo kama ikitangazwa itakuwa kivutio kikubwa kwa watalii.

Alimwomba pia kuigawanya wilaya hiyo mara mbili ili wananchi wa eneo hilo wapate huduma za utawala kwa urahisi.

Mwaka 2012 walianzisha Mkoa wa Katavi ikiwa na kilomita za mraba 47,000 eneo ambalo ni kubwa na kwamba kuna haja ya kuigawanya wilaya hiyo.

**Imeandaliwa na Neema Hussein na Jenifer Gilla**

# Mgombea TLS ajigamba kudhibiti ufujaji fedha

**Na Grace Gurisha**

MGOMBEA urais wa Chama cha Wanasheria Tanzania (TLS), Emmanuel Muga, amesema kipaumbele chake cha kwanza ni udhibiti ufujaji wa fedha za chama, kwa sababu wanachama wanaongezeka kila mwaka, lakini fedha hazionekani.

Aidha, amesema siku 30 za mwanzo wa utawala wake atahakikisha wanaweka mfumo wa fedha mudhubuti unaotumia teknolojia, ili fedha ikilipwa inaonekana kiasi kilichotolewa kwa ajili ya kuongeza uwazi zaidi.

Muga ambaye amewahi kuwa mwandishi wa habari alisema hayo jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu vipaumbele vyake kama atachaguliwa kwenye nafasi hiyo kubwa ikiwa ni kuhakikisha ada za wanachama zinaleta mabadiliko ya kweli ndani ya TLS.

Alisema hivi sasa wanachama wana malalamiko mengi kuhusu fedha zinavyotumika na kwamba ataweka mifumo ya kuhakikisha hakuna ufujaji na huo ndio utakuwa mwisho wa matumizi mabaya ya fedha za wanachama.

Muga ambaye alikuwa mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam kati ya mwaka 2019-2021, aliwaunganisha wanachama kuwa kitu kimoja na kusema akiwa rais atafanya mambo makubwa zaidi ya waliyoyafanya kwa kipindi hicho.

Alisema udhibiti wa fedha utakuwa kati ya vipaumbele vyake vya muda mfupi ambavyo pia vitahusisha kuleta umoja miongoni mwa mawakili, kusimamia nidhamu za mawakili na kulinda hadhi na taswira ya sheria.

Pia alisema kamati zao ndio zitakazoshughulikia masuala ya maadili ya mawakili, hawatasubiri mawakili wahukumiwe na kamati ya mawakili inayoongozwa na Jaji Ntemi Kilekamajenga.

"Hivi sasa chama kimegawanyika sana, hata katika ngazi ya uongozi ulipo sasa, nitachukua hatua kuhakikisha mawakili wanaungana na kufanyakazi kwa kuheshimiana kwa mujibu wa kanuni na taratibu za taaluma zinavyotaka," alibainisha Muga.

Pia alisema atakuwa na mpango mkakati wa miaka mitano unaoakisi kazi na malengo ya TLS kama yalivyo kwenye sheria, mpango huo utaangalia jamii ya Watanzania katika masuala ya sheria na namna nzuri ya kutimiza wajibu wake kwa mahakama.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Ajali ilivyoua wawili, kujeruhi 16

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

WATU wawili wamefariki dunia na wengine 16 kujeruhiwa baada ya basi walilokuwa wakisafiria kugonga nguzo ya daraja na kutumbukia mtoni.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Gallus Hyera, alithibitisha jana kutokea kwa ajali hiyo iliyohusisha basi la Kampuni ya Ngasere High Class lenye namba za usajili T 547 ECX lililokuwa likitokea Dodoma kuelekea mji wa Tunduma, mkoani Songwe.

Akielezea tukio hilo alisema, baada ya basi kufika katika eneo la mteremko mkali katika Kijiji cha Myovizi, wilayani Mbozi lilimshinda dereva na kwenda kugonga nguzo ya daraja kisha kutumbukia mtoni na kusababisha vifo hivyo na majeruhi.

Kamanda Hyera alisema katika ajali hiyo watu wawili walifariki dunia papo hapo na wengine 16 walijeruhiwa na kukimbizwa hospitali.

Alisema majeruhi hao walipatiwa matibabu na kuruhusiwa huku majeruhi wawili wakibaki hospitalini kuendelea na matibabu kutokana na hali zao kuwa mbaya.

Kaimu Kamanda Hyera aliwataja waliofariki kuwa ni Henry Msakila (29) na Ipyana Mwaibambe (47), wote wakazi wa Mkoa wa Dodoma.

Aidha, Kamanda Hyera aliwataja majeruhi wawili ambao bado wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Vwawa iliyopo wilayani Mbozi kuwa ni dereva wa basi hilo, Salim Mlelwa (42), mkazi wa Iringa ambaye amevunjika ubavu mmoja na kondakta wake, Zainabu Bakari (19), mkazi wa Kondoa mkoani Dodoma.



Wafanyabiashara wa ndizi eneo la Kimara Mwisho wakitoa bidhaa zao baada ya kutangaziwa kuondoka eneo hilo ili kupisha kazi ya upanuzi wa ujenzi wa barabara ya Morogoro unaoendelea jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Makonda: Tangaza mhalifu, chukua dau 100,000/-

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda ametangaza dau la Sh. 100,000 kwa kila atakayepeleka taarifa za wanaofanya uhalifu kwa kutumia bodaboda.

Alitangaza dau hilo juzi jijini hapa wakati akitangaza mshindi wa mashindano ya pikipiki ya 'Samia Motocross championship'.

Alisema lengo la kuweka dau hilo ni kukomesha matukio ya wizi ambayo yanaendelea kushika kasi na kwamba utambuzi wa madereva bodaboda ambao wanazitumia kufanya uhalifu utafanyika ili kukomesha.

Kwa mujibu wa Makonda, taarifa hizo zinatakiwa ziwe za uhakika ndipo aliyetoa taarifa apewe fedha husika, lengo ni kuhakikisha mwisho wa mwezi huu matukio yote yanakoma.

Alisema vijana wa bodaboda amezungumza nao katika vikao vya ulinzi vya usalama na kuwaambia kuwa hataki kuona wizi na majambazi katika Mkoa wa Arusha.

"Wanaoiba pochi, simu na kujeruhi watu maarufu kama 'tatu mzuka' hawatoki mbali ni vijana wenzetu tunaishi nao mtaani tunawajua, kuanzia kesho kama unamjua una uhakika na taarifa zake kuwa ni mwizi anachafua heshima ya bodaboda Mkoa wa Arusha ambao tunawapenda njoo ofisini kwangu ama kwa Mkuu wa Wilaya," alisema.

Makonda alisema mwananchi akiwa na taarifa hiyo atakuwa na faida tatu ya kwanza rafiki wa serikali, atapatiwa Sh. 100,000 na atalindwa.

"Nataka huu mwezi uwe wa mwisho kuwa na wezi ndani ya Mkoa wa Arusha wanaoiba tunawafahamu tunaishi nao wanachafua heshima ya mji wetu na sisi hatuwezi kukubali kuchafuliwa heshima hiyo."

"Wewe tuambie jina lake huyo mhalifu na kama ni mtu wa bodaboda tutajie namba yake ya bodaboda na sehemu anayopaki ukitupa taarifa za uhakika laki moja yako unayo ukikaa kijiweni siku nzima hujapata mteja na mwizi unamjua njoo ujichukulie laki yako tuachie mwizi."

Alisema wanataka Jiji la Arusha, watalii na wananchi wanatembea kwa amani bila kuona uhalifu.

Aidha, taarifa zitakazotolewa zitakuwa siri hakuna atakayevujisha na kusisitiza lazima taarifa ziwe sahihi, ili wamalizane na wezi na Agosti Mosi, mwaka huu, muda wa kufanya biashara uongezeke hadi saa sita usiku.

Aidha, alisema hawataki Mkoa wa Arusha anataka uwe ni wa kisiasa, kiuchumi na unaosukuma maendeleo ya mtu mmoja, familia yake kwa ujumla, taifa na kuwa na wananchi wenye afya njema.

"Siasa tumewaachia mikoa mingine huu mkoa hatutaki upoe kila mwezi una matukio kuna Land Rover Festival mpaka sasa wamejisajili magari zaidi ya 700 tunafanya utalii tunajiingizia fedha na wananchi wananufaika kiuchumi," alisema Makonda.

# Waziri: NEMC toeni vibali ndani ya mwezi mmoja

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji, amelitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kuhakikisha wawekezaji wanapata vyeti vya tathmini ya athari ya mazingira (EIA) ndani ya mwezi mmoja.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki Mikocheni jijini Dar es Salaam, alipotembelea ofisi za Baraza hilo kuzungumza na wafanyakazi na kuwapa maelekezo ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

Aidha, aliahidi kuwaondoa watumishi watakaokwamisha shughuli za uwekezaji kwa urasimu.

Alisema hatafurahi kuona wawekezaji wanazungushwa kupata vyeti hivyo vitakavyowasaidia kuanza uwekezaji wao na kwamba mtumishi atakayejaribu kuwakwamisha atakutana na adhabu kali kutoka kwake.

Dk. Kijaji alisema Rais Samia Suluhu Hassan, anafanya jitihada kubwa kutafuta wawekezaji maeneo mbalimbali duniani hivyo atashangaa kuona wasaidizi wake wanawakatisha tamaa wawekezaji hao kwa urasimu.

"Mimi sitakubali kuwa sehemu ya kukwamisha juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, katika kutafuta wawekezaji wanaokuja kuwekeza hapa nchini, tuweke muda mtu akiomba cheti hata siku 30 tuwe tumetoa na mwekezaji akaanza kufanyakazi, kama ananyaraka zote kwanini tumkwamishe," alisema.

Aidha, alisema mtu anayejaribu kukwamisha wawekezaji anawakwamisha Watanzania kwani mwekezaji anapoweka mradi anatengeneza ajira kwa wananchi na kuongeza kuwa hata kama mwekezaji huyo ana upungufu basi NEMC ndiyo yenye wajibu wa kumsaidia kurekebisha.

"Wawekezaji wengi wanakopa benki wanakuja kuwekeza mnawakwamisha sasa jiweke kwenye nafasi hiyo, kama inawezekana mwambie inawezekana na kama haiwezekani mwambie haiwezekani, lakini siyo kumzungusha kila siku mpaka anachoka," alisema.

"Kwa bahati nzuri mimi huwa nafuatilia sana na nitahakikisha yeyote anayejaribu kukwamisha mwekezaji nitamshughulikia na hata huko nilikotoka nimewashughulikia sana watu. Shirika la Maendeleo (NDC) wananijua sana shirika lilikuwa linakaribia kufutwa kwa kufanya vibaya lakini niliwanyoosha mpaka sasa limesimama," alisema.

Aliitaka NEMC kusimamia sheria na kuhakikisha mifuko ya plastiki hairejee tena kwenye matumizi kwani wananchi wanalalamika kwamba mifuko hiyo hivi sasa imejaa masokoni kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

"Nikiwa kwenye mkutano huu huu nimetumiwa ujumbe na mwananchi analalamika kwamba mifuko hii imejaa kila kona, lakini sisi tupo kwanini tusichukue hatua kwa wanaozalisha. Kama ilizuiwa kwanini inarudi tena wakati sheria zipo na tuliipiga marufuku," alisema.

## Mbaroni madai kupora dhahabu ya millioni 107/-

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU 14 wakazi wa vijiji vinavyozunguka mgodi wa Barrick North Mara uliopo Nyamongo wilayani Tarime, mkoani Mara, wanashtakiwa kwa kupora mawe ya dhahabu yenye thamani ya Sh. milioni 107.27 pamoja na uharibifu wa mali za mgodi zenye thamani ya Sh. milioni 18.78.

Akisoma mashtaka hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya, Stanley Mwakihaba, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Devis Katesigwa, alidai watu hao wanakabiliwa na kesi mbili za jinai.

Washtakiwa hao ni Kerembeta Mwita, Elias Mkami, Charles Rhobi, Wangubo Waitara, Hosea Hezron, Charles Mgaya, Mrimi Marwa, Rhobi Marwa, Pius Singa na Marwa Nyamhanga, Aprili 26, 2024 wakiwa na kundi la watu waliokuwa na silaha za jadi walivamia mgodi huo na kupora mawe.

Katsigwa alidai katika uvamizi huo yaliporwa mawe ya dhahabu yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 107.27 na kuharibu mali za mgodi huo zikiwamo nyaya za umeme na uzio zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 18.789.

Alidai makosa mengine katika shtaka hilo ni pamoja na yanayowakabili washtakiwa wengine waliomo katika orodha hiyo ambao ni Rhobi Marwa, Pius Singa na Marwa Nyamhanga waliosomewa shtaka la kuharibu mali uzio na nyaya za umeme yenye thamni ya Sh. milioni 13.3.

Washtakiwa hao walikana mashtaka yao na kuomba dhamana, lakini Mwanasheria wa Serikali, Devis Katesigwa alipinga dhamana yao na kudai kuwa tuhuma wanazokabiliwa ni za uvamizi, kujeruhi unyang'anyi wa kutumia silaha.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Mwakihaba aliungana na ombi la Mwanasheria wa Serikali kuamua watuhumiwa wote kwenda mahabusu hadi Julai 22, mwaka huu, kesi itakapotajwa.

# Wanufaika 400,000 wa TASAF kuondolewa kundi la ufukara

**Restuta James na Faustine Felician,** ARUSHA

WANUFAIKA 400,000 ambao wameshatoka kwenye kundi la ufukara (umaskini uliokithiri) nchini, wanatarajiwa kuondolewa kwenye mpango wa ruzuku ya kunusuru kaya maskini, unaofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Wanufaika hao ni miongoni mwa Watanzania 5,195,605 wanaoishi katika umasikini uliokithiri.

Hayo yalielezwa jana jijini hapa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shedrack Mziray, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema wanufaika hao wataondolewa kwenye mpango wa TASAF, baada ya kufanyiwa tathmini na kujiridhisha kwamba wanaweza kujitegemea.

Alisema mpango wa kunusuru kaya masikini umejikita kuwaokoa na kuwajengea uwezo wa kiuchumi ili zile zenye watu wanaoweza kufanyakazi, wajitambue na kuwepewa ruzuku ya kuanzisha biashara.

"Kaya hazitakiwi zikae kwenye mpango milele. Utaratibu unataka kwamba tukishawatambua tuwaondoe kwenye umasikini uliokithiri. Tunawawezesha kiuchumi, kukuza kipato cha kaya na kutengeneza rasilimali watu," alisema.

Mziray alisema katika kipindi cha pili cha TASAF Awamu ya Tatu kilichoanza mwaka 2020, kinatarajiwa kumalizika mwakani na Dola za Marekani milioni 883 (takribani Sh. trilioni mbili), zitatumika kuzinusukuru kaya hizo zinazoishi chini ya mstari wa umasikini.

Alisema fedha hizo ni mkopo wa Dola za Marekani 650 kutoka Benki ya Dunia (WB) na michango ya wadau wa maendeleo kutoka Jumuiya ya Ulaya (EU), Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN), serikali ya Sweden, Ireland, Norway na Dola milioni 50 kutoka Umoja wa Nchi zinazouza zaidi mafuta duniani (OPEC).

Alisema kati ya wanufaika 5,195,605, asilimia 55.7 ni wanawake na 44.3 ni wanaume.

Hata hivyo, alisema kaya zenye watu wenye ulemavu hazitaondolewa kwenye mpango huo.

Mkurugenzi wa Miradi wa TASAF, John Stephen, alisema takwimu za sensa zinaonyesha kwamba asilimia nane ya Watanzania wanaishi katika lindi la umasikini.

Alisema mpango wa TASAF wa uboreshaji wa kipato, unatolewa kwa walengwa wote wenye uwezo wa kufanya kazi ili kukuza ajira binafsi na ujira.

"TASAF inasaidia zaidi uwekezaji huu kwa ujuzi wa kukuza biashara na mafunzo ya kiufundi. Jumla ya vikundi vya akiba vya wanufaika 60,327 vyenye wanachama 838,241 vimeundwa. Kiasi cha akiba katika vikundi ni Sh. 7.9 bilioni. Kati ya akiba hizo, Sh. bilioni 3.2 zilitolewa kama mikopo kwa wanachama kwa ajili ya kuwekeza katika shughuli zao za kuwaingizia kipato," alisema.

Alisema kupitia mpango huo, kaya 83,666 zimepewa Sh. bilioni 17.1 kama ruzuku ya tija ya kujikimu, mafunzo na ushauri wa biashara ambazo zimefanikiwa kuanzisha miradi midogo ya kuwaingizia kipato.

Naye Meneja Mawasiliano kwa walengwa, Philipine Mmari, alisema kwa mujibu wa sensa na utafiti, halmashauri zote nchini zimefikiwa na miradi ya TASAF japokuwa maeneo yenye umasikini uliokithiri ni mikoa ya Pwani, Mtwara, Lindi, Unguja, Pemba na Kanda ya Ziwa.

Ili kuepuka udanganyifu na kuhakikisha TASAF inapata watu sahihi, alisema walengwa wanachaguliwa na wananchi katika maeneo yao katika ngazi ya kijiji.



Wasichana wakiwa kazini katika kiwanda cha kutengeneza suruali za 'jeans' jijini Dar es Salaam. Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa (GEF), ambayo ilitembelea kiwanda hicho mwishoni mwa wiki ilikipongeza kwa kuzingatia usawa wa kijinsia kwenye ajira. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Mwisho maboresho Luku za zamani Novemba 24

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema litafanya maboresho ya mfumo wa Luku na Novemba 24, mwaka huu ni mwisho.

Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa TANESCO, Irene Gowelle, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema wanatarajia Julai 22, mwaka huu maboresho hayo yataanza katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Alisema ni muhimu kwa wenye utaratibu wa kununua umeme na kutunza kuuingiza kwenye Luku kabla ya maboresho kwa kuwa inaweza kujitokeza changamoto na kwamba watakapohakikisha umeshaingia ndipo waingize tokeni za maboresho ya mfumo wa Luku.

"Tunasisitiza hilo kwa sababu kutokufanya hivyo kutasababisha mteja kupoteza umeme wake iwapo ataanza kuingiza tokeni za maboresho ya mfumo wa Luku kabla ya umeme wake wa zamani.

"Maboresho haya ni kwa ajili ya kuongeza ufanisi, usalama na kuendelea kuwa na kumbukumbu nzuri za matumizi na manunuzi ya umeme kwa mteja."

"Ndio maana tunaona ni vyema tuwataarifu wateja mapema kwa ajili ya kuepusha usumbufu kama kukosa huduma, wafanye zoezi hili tukishirikiana nao kwa pamoja ili mita zote ziwe na viwango vya kimataifa," alisema Irene.

Aidha, alieleza kuwa maboresho hayo yatakapoanza mteja baada ya kununua umeme atapokea makundi matatu yenye jumla ya tarakimu 60, na kwamba kila kundi litakuwa na tarakimu 20 na mawili ya mwanzo ni kwa ajili ya maboresho na la mwisho litakuwa ni umeme ambao atakuwa amenunua.

Alisema mteja ataingiza makundi yote ya tarakimu kwa kufuata mpangilio kama utakavyokuwa unasomeka kwenye risiti ya malipo, baada ya hapo atakuwa amekamilisha kufanya maboresho na kuingiza umeme wake alionunua.

Hata hivyo, alisema ziko baadhi ya changamoto ambazo wanazipokea kutoka kwa wateja wao katika maeneo ambayo tayari walishapita, ikiwamo uelewa mdogo unaosababisha wengine kuingiza namba za tokeni bila kufuata mpangilio jambo linalosababisha kushindwa kufikia mwisho wa kufanikisha maboresho.

Vile vile, alisema ziko baadhi ya mita zinakataa tokeni za maboresho na alitoa rai kwa wananchi watakao kutana na changamoto hiyo wawasiliane na TANESCO kupitia namba za huduma kwa wateja ili wapatiwe msaada.

Alisema kwa Mkoa wa Temeke namba za huduma kwa wateja ni 0694169798, Kinondoni Kusini 0756251753, Ilala 0733212575, Kinondoni Kaskazini 0692768587, Pwani 0738256237.

"TANESCO tumejipanga vizuri katika ofisi zetu na kuhakikisha kwamba tunaweza kuwasaidia Watanzania, na tayari elimu imeshaanza kutolewa juu ya zoezi hilo, tunapita katika maeneo mbalimbali kuwafahamisha wananchi na kuwapa elimu ni namna gani ya kufanya maboresho haya," alisema Irene.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waacheni watoto wa kike watimize ndoto zao msiwazalishe mapema

**WAKATI** Rais Samia Suluhu Hassan akiwa ameanza ziara yake katika Mkoa wa Katavi kukagua shughuli mbalimbali za maendeleo na kuzindua miradi, pia ametembelea Hospitali ya Rufani Mkoa wa Katavi na kushuhudia watoto waliojaa hospitalini hapo wakiwa wamejifungua watoto wenzao.

Kwa mshtuko Rais Samia, alishuhudia wengi wa wazazi kwenye wodi hiyo wakiwa na umri kati ya miaka 15 na 19.

Ukiangalia umri huo ni wa watoto ambao wanapaswa kuwa shuleni, lakini ndoto zao zimezimwa na sasa wamekuwa wazazi wa kulea watoto wenzao.

Kujifungua mtoto ukiwa na umri mdogo kuna athari nyingi kwa sababu viungo vinakuwa havijakomaa na wengi wao huishia kufanyiwa upasuaji kutokana na kushindwa kuhimili mikikimikiki ya uzazi.

Athari nyingine ni kuchanika kwenye njia ya uzazi na matokeo yake kupata tatizo la ugonjwa wa fistula.

Wataalamu wengi wa afya wanaamini kuwa umri sahihi wa mwanamke kupata ujauzito ni kuanzia miaka 20 hadi 35 ambapo viungo vyake vinakuwa vimeshakomaa.

Hata hivyo, watoto wengi wa kike hasa wa vijijini wanalazimika kujifungua katika umri mdogo kwa kujiingiza katika mahusiano wakiwa katika umri mdogo au wengine kulazimishwa ndoa za utotoni na wazazi.

Wengine hupata mimba kwa kubakwa na kulazimika kupata mtoto akiwa na umri mdogo. Matukio ya mabinti kuzaliwa katika umri mdogo yanaathiri ndoto zao za kufikia maisha wanayoyapenda wakiwa wakubwa.

Sheria ya Ulinzi wa Mtoto, 2009 inazuia mtoto (umri chini ya miaka 18) kutekeleza majukumu ya mtu mzima.

Aidha, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inamzuia mtoto chini ya miaka 15 kuolewa na sheria hii ilikuwa na lengo la kumlinda mtoto asipewe majukumu ya kulea familia akiwa na umri mdogo.

Rais Samia alipotembea Hospitali ya Katavi, alibaini kuwa ni mama mmoja tu ndiye aliyepevuka ambaye alikuwa na miaka 22, lakini wengine wote walikuwa kati ya miaka 15 na 19 na hao walikuwa wamejifungua watoto ambao hawajatimiza siku zao za kuzaliwa (njiti).

Kwa kuonesha kusikitishwa na alichokikuta, aliwaomba wananchi wa Mkoa wa Katavi, kuwapa nafasi watoto wa kike waweze kusoma na kutimiza malengo yao na hata wafikie umri unaostahili angalu ajifungue akiwa amefikia umri wa miaka 19 na kuendelea, lakini sio kwa hali aliyoikuta hospitalini hapo.

"Ujumbe huu ni kwenu wananchi mliopo hapa na wale ambao wananisikiliza kupitia vyombo vya habari, tujitahidi kuwapa nafasi watoto wa kike wapate elimu, wapevuke kabla ya kuolewa au kupewa ujauzito, hilo ninaomba sana sana."

Ushauri na ombi alilotoa Rais Samia ni amri ambayo inatakiwa itekelezwe kote nchini, kwa sababu vitendo vya kukatisha ndoto za watoto wa kike kuendelea na masomo vimekuwa vikifanyika sana katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na mikoa ya Kusini.

Changamoto wanayokutana nayo wazazi hao wadogo ni kutelekezwa na watu waliowazalisha na kuwaachia mzigo wa malezi wazazi wa watoto hao ambao nao wengi wao hawana uwezo.

Matokeo yake ni watoto kupata utapiamlo na udumavu kwa kukosa chakula bora.

Watoto wa kike waachwe wasome, wasizalishwe wakiwa wadogo, waacheni watimize ndoto zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Udanganyifu mitihani unavyokuwa mazoea

**WATAHINIWA** 24 wa mtihani wa taifa wa kidato cha sita, wamefutiwa matokeo kutokana na kile kinachoelezwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), kuwa ni kufanya udanganyifu kwenye mtihani huo.

Baraza hilo linawataja watahiniwa waliofutiwa matokeo ya mtihani huo kuwa ni wale waliobainika kuingia na simu katika vyumba vya mtihani, huku wengine wakiwa na notisi na wengine wakisaidiana kufanya mitihani.

Idadi hiyo ya waliofutiwa matokeo ya mtihani huo, imekuwa kubwa zaidi kuliko ya mwaka jana, kwani mwaka huo baraza lilitangaza kufuta matokeo ya watahiniwa 11, sababu ikiwa kufanya udanganyifu.

Katika matokeo ya mtihani huo wa kidato cha sita kwa mwaka 2022, watahiniwa 15 walifutiwa matokeo bado sababu kuu ikiwa ni ya udanganyifu ambao inaonekana haujapatiwa suluhisho la kudumu.

Nimejaribu kukumbishia miaka michache ya nyuma, lakini inaonekana kila mwaka ambao baraza hilo limekuwa likitangaza matokeo, huwa kuna watahiniwa wanaofutiwa matokeo kutoka na sababu hizo.

Mtindo huo utaendelea hadi lini? Lengo lake ni nini? Kwa nini mwanafunzi akubali kufaulu kwa udanganyifu badala ya kutumia elimu aliofundishwa darasani? Mwisho wa udanganyifu ni nini?

Udanganyifu katika mitihani ni janga ambalo linaangamiza elimu ya Tanzania kimya kimya likiwa limejificha, hivyo tukiridhibiti, tutakuwa tumeokoa elimu inayotishiwa na vitendo hivyo.

Mtindo au tabia hiyo ya wizi na udanganyifu wa mitihani, vimekuwa vikiporomosha elimu, kutokana na ukweli kwamba, wanafaunzi wanaofaulu kwa njia hiyo, hawawezi kufika mbali kielimu.

Kama ni kukemea wizi huo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilishakemea sana, ninadhani kilichobaki ni kuchukua hatua ambazo zitawafanya wahusika waogope kufanya udanganyifu.

Wizara isiishie kukemea kwa kutumia vyombo vya habari, badala yake ichukua hatua kali kwa wahusika, ili kuwa fundisho kwa wahusika na hata kwa wengine wanaojipanga kufanya udanganyifu.

Udanganyifu ukifanyika, uchunguzi ukawabaini wahusika, ni vyema wasiishie kufutiwa kisha wakapangiwa siku nyingine ya kufanya mtihani, badala waadhibiwe kulingana na makosa yao.

Vinginevyo vitendo vya udanganyifu vitaendelea kuripotiwa kila matokeo yanaotangazwa kana kwamba imeshindikana kuwadhubiti wanaoshiriki mchezo huo mchafu unaporomosha elimu.

Wiziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda, aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema, wizara imebaini kuwa baadhi ya watumishi wa umma wasio waaminifu hushiriki vitendo hivyo, na kwamba vitendo hivyo ni sawa na uhujumu uchumi.

Sasa kama ni sawa na uhujumu uchumi, basi ni vyema wahusika wanaobaibika kukutwa na hatia, wahukumie kulingana na jinsi adhabu za uhujumu uchumi zilivyo, ili kukomesha udanganyifu.

Si sahihi kuendelea kufumbua macho wahujumu uchumi, badala yake wachukuliwe hatua stahiki, ili kulinda elimu isiendelee kuporomoka kutokana na tamaa ya watu wachache.

Ikumbukwe kuwa, matatizo katika ubora wa huduma nchini, yanagusa sekta zote, ikiwamo elimu, hivyo, wakati serikali ikiwa na wajibu wa kupanga, kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa mipango yote ya maendeleo, ni muhimu kukumbushana umuhimu wa elimu katika kuchochea maendeleo ya sekta nyingine.

Vilevile udanganyifu katika mitihani una madhara mengi, ikiwamo kuzalisha wataalamu wasiokuwa na viwango, kutokana na wamewezesha bila kuwa na sifa za kustahili kuendelea na masomo.

Hivyo, NECTA na serikali kwa ujumla ni muhimu kuongeza au kubuni mikakati zaidi ya kupambana na watu ambao wanafanya udanganyifu kwenye mitihani, ikiwamo kuwabaini wasimamizi na walimu anbao hushirikiana kwa namna moja au nyingine kufanya udanganyifu huo.

## Wanachama 37 CHADEMA watimkia ACT-Wazalendo

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANACHAMA 37 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mkoani Lindi, wakiwamo viongozi watano wametangaza kukihama na kutimkia ACT-Wazalendo kwa madai ya kuchoshwa na migogoro inayoendelea.

Viongozi hao ni wenyeviti ngazi ya mkoa na wilaya, katibu na mweka hazina ambao wamejiunga na ACT- Wazalendo wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Makonde, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Viongozi waliokabidhiwa kadi na Makamu Mwenyekiti Taifa, ACT-Wazalendo, Isihaka Mchinjita ambaye ni Mwenyekiti na Katibu ngazi ya mkoa, Zainabu Lipalapi na Mussa Rugoshwela na Mwenyekiti wa Vijana wa CHADEMA wilaya, Dowa Omari, Mwenyekiti wa Baraza la Wazee mjini Lindi, Bakari Likapu na Mweka Hazina wa Jimbo, Mohamedi Mandowe.

Akizungumza baada ya kutangaza uamuzi huo, mwanachama, Mussa Rugoshela, alisema ni pamoja na migogoro inayoendelea kufukuta ndani ya CHADEMA ambayo inarudisha nyuma jitihada za kuleta ukombozi wa kweli wa Watanzania.

Wanachama hao 37 kabla ya kujiunga na CHADEMA walikuwa Chama cha Wananchi (CUF), ambapo walijiondoa kufuatia mgogoro ulioibuka kwa Mwenyekiti Profesa Ibrahim Lipumba kujiuzulu kisha kurejea tena kupitia nguvu ya mahakama.

Akiwakaribisha ACT-Wazalendo, Mchinjita aliwapongeza wanachama hao kwa uamuzi waliochukua kujiunga nao kwa kuwa kutaimarisha nguvu katika mapambano ya ukombozi ndani ya Jimbo la Lindi na mkoa kwa ujumla.

"Nasema karibuni sana kazi iliyopo mbele yetu ni uchaguzi kuanzia ngazi za mitaa unaotarajia kufanyika mwaka huu, na ule mkuu utakaofanyika mwaka kesho 2025, hivyo kujiunga kwenu kutaongeza chachu ya ushindi," alisema Mchinjita.

**Wanachama hao 37 kabla ya kujiunga na CHADEMA walikuwa Chama cha Wananchi (CUF), ambapo walijiondoa kufuatia mgogoro ulioibuka kwa Mwenyekiti Profesa Ibrahim Lipumba kujiuzulu kisha kurejea tena kupitia nguvu ya mahakama.**



Mbunge wa Mbarali, Bahati Ndingo (kulia), akisalimiana na mmoja wa wakazi wa kijiji cha Lwalanji, Kata ya Igawa mkoani Mbeya jana, alipofika kijijini hapo kusikiliza na kutatua kero za wananchi ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kutembelea kijiji kwa kijiji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wataka ushirikiano kuchochea matumizi nishati umeme kwenye kilimo

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI serikali ikisisitiza matumizi ya nishati safi ili kulinda afya za Watanzania, sekta ya kilimo imeonekana kuachwa nyuma licha ya kuwapo rasilimali jua, sababu kuu ikitajwa kuwa ni uelewa mdogo wa matumizi ya nishati hiyo.

Ili kukabiliana na tatizo hilo, wadau wa habari wameshauri taasisi binafsi kushirikiana na vyombo vya habari kuongeza kasi ya uandishi wa habari za matumizi ya nishati hiyo, kwa ajili ya kuongeza uelewa na uhamasishaji wa matumizi katika kilimo.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Uandishi wa Habari za Nishati ya Umeme Jua katika Kilimo katika Nchi za Afrika na Mashariki kwa mwaka 2023, iliyoandaliwa na Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC) kwa kushirikiana na Kituo cha Ubora wa Vyombo vya Habari Afrika (ACME).

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Elisha Magolanga, alisema kuna haja ya taasisi hizo kushirikiana kuomba fedha za kuendesha miradi ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuhusu uandishi wa habari za nishati ya umeme jua kwenye kilimo.

Alisema waandishi wa habari wanashindwa kuandika habari hizo kwa kina kwa sababu hawana uelewa wa kina kuhusu suala hilo na fedha za kutosha kugharamia utekelezaji, hasa katika kipindi hicho ambacho vyombo hivyo vinapitia anguko la kiuchumi.

"Hali hiyo inasababisha waandishi wengi kuandika habari zinazotokana na matukio yaliyoandaliwa na mashirika binafsi hali inayosababisha kukosekana habari za kijamii katika eneo hilo ambazo ndio zina wasomaji wengi," alisema.

Aidha, alisema kupitia ushirikiano huo waandishi wa habari watapewa mafunzo na kuwezeshwa kiuchumi na kutembelea maeneo mbalimbali miradi ya umeme jua kwenye kilimo inakotekelezwa na kuandika habari zitakazoleta hamasa kwa wakulima wengine kuiga mfano.

Alishauri pia kuwapo na mafunzo ya ndani ya vyumba vya habari mara kwa mara kwa kushirikisha taasisi zilizojikita katika eneo husika, ili kuwapo na waandishi waliobobea na kuandika habari kwa weledi.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN), Salome Kitomari alisema waandishi wa habari wakiwezeshwa kielimu na kiuchumi, wataandika habari za zitakazoleta uchechemuzi na kuzisaidia jamii za wakulima kusonga mbele kimaendeleo.

Alisema kwa sasa elimu itakayotolewa kwa waandishi wa habari inapaswa pia kuzingatia mabadiliko ya teknolojia, ili taarifa zitakazotolewa ziyafikie makundi yote hasa vijana ambao ndio wanategemewa kuwa watumiaji wakubwa wa nishati hiyo kwenye kilimo.

Aidha, alishauri pia kuwapo na uandishi wa habari wa ushirikiano katika nchi, ili kuwapo na mawanda mapana ya walaji wa habari vyombo vya habari vinufaike na habari iliyoandikwa kwa kuongeza mapato.

Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Mwananchi, Joseph Damas, alisema kwa kuwa baadhi ya habari ikiwamo za nishati ya jua hazitoki kwenye kurasa za mwanzo za gazeti kutokana na kutovutia wateja kuna haja ya utafiti unaofanyika kuonyesha namna ya kuziboresha ili zichangie kuingiza mapato.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania, Deodatus Balile, akifungua hafla hiyo alisema mafunzo yatakayotolewa kupitia mradi huo, yatawezesha waandishi wa habari kubobea katika eneo la nishati ya umeme jua na kilimo na kuongeza uwapo wa habari hizo katika vyombo vya habari.

Aidha, alisema mafunzo hayo yalenge kuwajenga, kujua umuhimu wa umeme jua na matumizi yake katika kilimo kama vile kukausha vyakula, na kilimo cha umwagiliaji ili wakaielimishe jamii.

Akiwasilisha matokeo ya utafiti huo, Mhadhiri wa SJMC, Darius Mukiza, alisema walichukua sampuli ya habari 63 kutoka kwenye vyombo vya habari maarufu katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.

Alisema utafiti huo ulionyesha kuwa kati ya vyombo hivyo, Uganda waliandika habari 30, Kenya 23 na Tanzania 10. Kati ya hizo kwenye runinga jumla zilikuwa 33 kwenye magazeti 29.

Hata hivyo, habari hizo hazikupewa kupaumbele katika kurasa za mbele za magazeti, utafiti ulionesha kuwa nyingi ziliwekwa kuanzia ukurasa wa tano na kuendelea.

Alisema utafiti unaonesha kuwa sababu za uhaba wa habari hizo ni waandishi kukosa uelewa wa sekta hiyo, uhaba wa rasilimali fedha kuwawezesha kwenda kutafuta habari, kukosa soko na wakulima kukosa uelewa wa matumizi ya umeme huo kwenye kilimo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





## Zimamoto yataja siri kudhibiti moto sokoni, shuleni

**Na Oscar Assenga,** TANGA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limesema siri iliyowawezesha kufanikiwa kudhibiti matukio ya moto kwenye maeneo ya masoko na shule mkoani Tanga ni utoaji wa elimu.

Limesema kila wakati limekuwa likitoa elimu ikiwamo hatua za awali za kuchukuliwa kukabiliana na majanga hayo yanapokuwa wakijitokeza.

Ofisa Operesheni wa Jeshi hilo mkoani hapa, Mrakibu Msaidizi, Yusuf Msuya, aliyasema hayo juzi mkoani hapa wakati wa mahojiano maalum na Nipashe.

Alisema mkakati ambao walifikiria ungeweza kuleta mafanikio ni utoaji wa elimu ambao jeshi hilo kwa kushrikiana na viongozi wa masoko na uongozi wa shule zenye bweni mkoani hapa kuhakikisha wanaweka mikakati ya pamoja kudhibiti vitendo hivyo.

"Kubwa zaidi ni kuwapa elimu ya kukabiliana na moto kwa viongozi wa masoko kuhakikisha wanakuwa na vifaa vya kuzimia moto na wale wafanyabiashara wamepewa mafunzo na kueleza madhara ya moto na namna ya kukabiliana nayo yanapokuwa yakitokea," alisema.

Aidha, alisema elimu hiyo wanaitoa pamoja na kuwaeleza lazima wahakikishe kwenye masoko kuna mpangilio mzuri, hususani kwa mama lishe kuwa na maeneo yao.

Huvyo, alitoa wito kwa viongozi wa masoko kuhakikisha wanaendelela kusimamia kanuni za kukabiliana na majanga ya moto kwa wafanyabiashara kwenye maeneo yao, ikiwamo yanakuwa salama.

Hata hivyo alisema kwamba hivi sasa wamefanikiwa kuanzisha klabu za zimamoto kwa shule za msingi na sekondari na wanachama wa klabu hizo wanakuwa mabalozi wazuri wa Jeshi hilo katika shule hizo na maeneo ya makazi.

Kadhalika, aliwataka wananchi wenye tabia za kupiga simu na kueleza habari zao binafsi ikiwamo utani kuacha mara moja kwani kufanya hivyo ni kosa.

Alisema: "Tunawataka waache kufanya hivyo kutokana na kwamba wakati wanapokuwa wameshikilia simu kwa kupiga na kueleza mambo yao binafsi ama utani inasababisha wananchi wenye matukio ya ajali za moto wanaotaka kuripoti kushindwa kufanya hivyo".

# Tabibu mbaroni tuhuma wizi wa dawa za mil.300/-

**Na Allan Isack,** NGORONGORO

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, Murtallah Mbillu, amemsimamisha kazi Tabibu Msaidizi wa Zahanati ya Misigiyo, Samweli Panga, anayekabiliwa na tuhuma za wizi wa dawa na vifaa tiba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa waandishi wa habari na kitengo cha mawasiliano katika halmashauri hiyo, ilieleza kuwa Mbillu, amemsimamisha kazi Panga, ambaye ni Tabibu Msaidizi kwa kukamatwa na dawa na vifaa vya tiba.

Mbillu alisema alisema kwa sasa mtumishi huyo amesimamishwa kazi kupisha uchunguzi wa tuhuma hizo, endepo ikibainika ni za kweli hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mtumishi huyo wa serikali alikutwa na dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.milioni 344. 2.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, ilieleza kuwa Panga, alikutwa akiwa anauza vifaa tiba na dawa katika mnada wa Olbalbal wilayani humo Juni 13, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, kupitia taarifa hiyo Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, alisema kuwa mtumishi huyo alikamatwa baada ya kupata taarifa za siri na kuweka mtego.

Alisema baada ya kuwekwa mtego walifanikiwa kumkamata akiwa na vifaa vya tiba na dawa ambazo serikali inatumia gharama kubwa kununua kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa wananchi wa eneo hilo.

Hivyo, alitoa onyo kwa watumishi wote wa Halmashauri ya Ngorongoro, kufanya kazi kwa kufuata sheria, utaratibu na kanuni za utumishi wa umma.

Alisema endapo itabainika kuna mtumishi anahusika kutenda hujuma kama hiyo, hatosita kumchukulia hatua kali za kisheria bila ya kujali nafasi yake, kwa kuwa tabia ya wizi ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Dk. Libori Tarimo, akizungumzia suala hilo, alisema amelaani kitendo hicho na kusema hatomfumbia macho mhudumu yeyote wa afya atakayeenda kinyume na maadili ya kazi.

Alisema: "Serikali inatoa dawa na vifaa tiba ili vitumike kwa lengo lililokusudiwa na siyo vinginevyo, hivyo mhudumu anayekwenda kinyume na maadili ya kazi sitomfumbia macho hata kidogo."




Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka 2024, Geofrey Mnzava (katikati), akikata utepe kuweka jiwe la msingi kwenye mradi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wa Dambia Haydom wilayani Mbulu mkoani Manyara, wenye thamani ya Sh. bilioni 41.2 utakaonufaisha vijiji 21 vyenye watu 133,737 juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# TANAPA, FDH waingia makubaliano kuvutia watalii

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Foundation For Disabilities Hope (FDH), wameingia makubaliano ya kuhamasisha watu wenye ulemavu kutoka ndani na nje ya nchi kutembelea vivutio vya utalii.

Makubaliano hayo yanalenga kulisaidia taifa kupata mapato ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kutangaza vivutio vilivyopo nchini.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi FDH, Mozzah Mauly na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Maiko Salali, walifanya makubaliano hayo juzi walipotembelea makao makuu ya TANAPA mkoani hapa.

Makubaliano hayo yalifanyika katika kikao kilichohudhuliwa na Kamishna wa Uhifadhi Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Juma Kuji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi FDH, Mozzah Mauly, alisema pamoja na mambo mengine kikao hicho kililenga kudumisha uhusiano uliopo kati ya TANAPA na FDH.

Pamoja na mambo mengine, kikao hicho kilijadili masuala mbalimbali kuhusu watu wenye ulemavu ikiwamo kampeni iitwayo 'Niache niishi' na utalii jumuishi" ambayo itahamasisha watalii kwenda hifadhi za taifa.

Alisema dhima ya FDH ni kuhamasisha watu wenye ulemavu kutoka ndani na nje ya nchi kutembelea vivutio vya utalii na kuliongezea mapato taifa kupitia vivutio mbalimbali.

Aidha, katika kikao hicho uongozi wa FDH na wafanyakazi wake walitembelea makao makuu ya TANAPA, lengo likiwa ni kujifunza mambo mbalimbali.

Vilevile, FDH ilimkabidhi cheti cha pongezi na tuzo Kamishna wa Uhifadhi TANAPA, Juma Kuji, kwa kutambua mchango wa shirika katika kusaidia watu wenye ulemavu na makundi maalum katika jamii.

Awali, Mkurugenzi wa FDH, Maiko Salali alilipongeza TANAPA kwa kazi kubwa ya kusimamia maliasili za taifa pamoja na kusaidia watu wenye ulemavu katika jamii.





# Kigogo wa CCM aonya makandarasi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, amewaonya baadhi ya makandarasi wa ujenzi wa barabara za Halmashauri ya Ushetu kutengeneza kwa kiwango cha chini ili waendelee kunufaika na fedha zinazotolewa na serikali.

Mabala alitoa onyo hilo juzi katika mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Charahani kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili wananchi katika Kijiji cha Nhimbo.

Alisema makandarasi hao wamekuwa wakijenga barabara chini ya kiwango na wanapohojiwa na wananchi wanajibu wanafanya hivyo ili waendelee kupewa zabuni na kunufaika na fedha hizo za serikali.

Alisema ataendelea kufanya utafiti ili kuwabaini na kuwawajibisha makandarasi wa aina hiyo kwa sababu wanaitia hasara serikali kutokana na vitendo vyao hivyo.

Mbunge huyo aliendelea kusema licha ya uzembe na kauli hizo, makandarasi hao wamekuwa hawafuati makubaliano na sheria za mikataba yao kwa kuajiri wananchi kutoka nje ya wilaya hiyo hata kwa kazi zisizohitaji ujuzi wa elimu.

"Katika kata hii barabara zinajengwa pasipo mitaro na madaraja maeneo yasiyo sahihi tena chini ya kiwango na yanaharibika kwa muda mfupi, wakiulizwa na wananchi wanajibu wakale wapi na bila kufanya hivyo hawawezi kunufaika na fedha za umma. Tutaanza kuwashughulikia ili kuondoa adha hii," alisisitiza Mabala.

Mbunge Charahani, alisema atawafuatilia makandarasi wanaotoa majibu yasiyofaa kwa wananchi ili wachukuliwe hatua na kunyimwa kazi ndani ya halmashauri hiyo.

Alisema atahakikisha barabara zilizoharibiwa na mvua zinarejeshwa katika hali yake na kurahisisha usafirishaji wa mazao mpaka sokoni hasa kwa kipindi hiki cha msimu wa pamba na tumbaku ili kuiongezea mapato ya ndani halmashauri yao.

Mkazi wa Chona, William Bundala, aliwaomba viongozi kuwabana makandarasi wanaotekeleza miradi ya maendeleo waendelee kupata kazi zisizohitaji ujuzi ili wapate fedha za kujikimu kimaisha na kuachana na michezo ya kubahatisha.

# Wafa wakishindana 'kufakamia' viloba

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAKAZI wawili wa mji wa Sirari, Tarafa ya Inchugu wilayani hapa Mkoa wa Mara, Chacha Mronya na Zakayo Marwa wanadaiwa kufa baada ya kunywa pombe kali za kwenye pakiti maarufu kama viroba zilizoingizwa nchini kinyemela kupitia mpaka wa Sirari.

Akisimulia tukio hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Wakuru Mirumbe alisema kuwa walikufa Julai 11, mwaka huu baada ya kunywa pombe hiyo katika mji wa Sirari.

"Mronya alikutwa amefariki baada ya kujilaza kwenye kiti ndani ya 'salon' baadaye mwingine ambaye ni Zakayo wakati akibishana na wenzake kuwa ni bingwa wa kunywa."

"Tunatoa wito kwa vijana kujiepusha na unywaji wa pombe ambazo hazina viwango na zinazoingizwa hapa nchini kinyemela kupitia njia za panya," alisema Mirumbe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, Michael Njera amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusisitiza kuwa wanaendelea na uchunguzi na kuwasaka wanaojihusisha na uuzaji wa pombe hizo zinazoingizwa kinyemela nchini.

"Tutafanya msako na tutawachukulia hatua kali za kisheria wote wanauza pombe hizo," alisema.

Kamanda Njera aliwashauri vijana kuacha kutumia vinywaji ambavyo havitathibitishwa ubora wake na mamlaka husika vinavyoingizwa nchini kinyemela.

# Mbunge akerwa rundo la kero ofisini

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MBUNGE wa Sengerema, Khamis Tabasamu ameonyesha kukerwa na utendaji kazi wa baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza hiyo kwa kusababisha kurundikiwa kero za wananchi ofisini kwake.

Tabasamu alitoa dukuduku lake hilo mwishoni mwa wiki iliyopita katika kikao kazi na watumishi wa halmashauri hiyo na kuwataka kubadilika kwa kufanya kazi kwa bidii na kutoa ushauri kwa wakuu wa idara na viongozi wa ngazi ya wilaya ili kuweza kutatua kero zinazowakabili wananchi ngazi za vitongoji na vijiji.

Alisema kumekuwapo na kero zinazowakabili wananchi hususani kwenye huduma za fya, elimu ambazo hazipatiwa ufumbuzi na kuwalazimu kuwasilisha katika ofisi yake ili zipatiwe ufumbuzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Binuru Shekidele aliwataka watumishi hao kufanya kazi kwa bidii na ubunifu ili kufikia malengo waliyojiwekea ikiwamo usimamizi wa mapato na miradi ya maendeleo.

Shekidele, alisema ataendelea kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wazembe kwa kukwamisha miradi ya maendeleo na shughuli nyingine za serikali.

Kwa upande wao, wakuu wa idara na vitengo vya halmashauri hiyo walieleza mipango yao ya utekelezaji wa majukumu katika idara zao na usimamizi wa watumishi waliopo chini yao, raslimali, miradi na ukusanyaji wa mapato.

Kikao hicho kilichojumuisha waratibu elimu, watendaji wa kata, wakuu wa sekondari, walimu wakuu wa shule za msingi na waganga wafawidhi wa vituo vya afya na zahanati.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, akikabidhi hati ya kiwanja kwa Immaculata Tenga, mkazi wa Ilemela anayedaiwa kufuatilia hati hiyo katika Halmashauri ya Ilemela kwa zaidi ya miaka tisa licha ya kufuata taratibu zote muhimu. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Wasotea hati za ardhi kwa miaka tisa

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

HATIMAYE baadhi ya wakazi wa Manispaa ya Ilemela wamepata hati za kumiliki viwanja kwa shinikizo la Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda baada ya kuzungushwa kwa zaidi ya miaka tisa.

Akizungumza baada ya kupata hati hiyo juzi, mmoja wa wakazi hao, Immaculata Tenga alisema kuwa: "Tangu mwaka 2015 nafuatilia hati, kila nikija ardhi wananiambia njoo kesho njoo kesho, nilifuatilia kwa muda mrefu bila mafanikio yoyote."

Immaculate, alisema siku moja kabla, Mkuu huyo wa Mkoa alifanya ziara ya kushtukiza katika manispaa hiyo na kubaini kuwapo kwa tatizo la ucheleweshwaji huo na kutoa saa 24 wakabidhiwe hati zao kutoka idara ya Ardhi.

Mjane Anna Andrew, alisema hati yake ameifuatilia kwa miaka miwili kutoka Dar es Salaam anakoishi hadi Mwanza bila mafanikio.

Anna, alisema kwa amri hiyo ya mkuu huyo wa mkoa, ameipata ndani ya siku moja.

Akizungumzia utekelezaji wa amri yake hiyo, Mtanda aliwataka watumishi wa Idara ya Ardhi katika manispaa hiyo kutatua kero za ardhi na kuwahudumia wananchi kwa haki na kwa wakati, vinginevyo watakuwa wanachafua taswira ya serikali.

"Uhusiano baina ya wananchi na serikali ni muhimu, mwananchi mmoja amefuatilia stakabadhi ya hati kwa miezi sita hapo ardhi, wanatengeneza mazingira ya kufanya jambo liwe gumu ili kuwakatisha tamaa wananchi, wanatengeneza wapate rushwa, hawa wanatugombanisha na wananchi," alisema Mtanda.


Ukurasa 12

'Wasioona wanafanya makubwa njooni VETA Dar mjithibitishie'


Ukurasa 13

Wanawake wakataa kupewa 'lifti', usawa kijinsia uwe taa kuiongoza nchi

Nipashe

TESA

Jumanne Julai 16, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


Ukurasa 14

Ushuhuda wanaoozwa utotoni wanavyoteswa

TEKNOLOJIA
NA BEATRICE PHILEMON

# Mbegu za migomba kwenye paketi zaja, huandaliwa kutoka kwenye ndizi mbivu

KWA wakulima wa migomba, hii ni habari njema kwao. Kwa sababu juhudi zinafanyika kuandaa mbegu za migomba ili zipatikane kwa wepesi na urahisi kama ilivyo kwa mbegu za mchicha au mahindi.

Ni kazi ya utafiti inayofanywa na Gerald Mabuto, mwanafunzi wa mwaka wa nne wa shahada ya menejimenti ya rasilimali, katika Chuo Kikuu cha Mzumbe-kampasi ya Mbeya.

Anasema utafiti aliofanya sasa umewezesha kupata mbegu za migomba kutoka kwenye ndizi zilizoiva na kuzalisha miche, lakini juhudi zinaendelea kuandaa mbegu ambazo zitakaushwa na kufungashwa kwenye paketi, japo anasema hatua hiyo haijafikiwa.

Akizungumzia lengo la utafiti anasema ni kuinua biashara ya ndizi na kuongeza kipato kwa kutumia miche ya migomba inayozalishwa kwa kutumia ndizi mbivu asilia kama malindi, mkono wa tembo, mshare na kisukari.

Mabuto, anasema ni teknolojia mpya inayotumia njia za asili kuzalisha mbegu ya mgomba tofauti na mbinu nyingine zilizotumiwa katika kilimo hicho ambazo ni pamoja na kung'oa chipukizi kwenye shina.

Anataja sifa za mbegu hizo kuwa zinatumia muda mfupi kukua na kutoa matunda, kuanzia miezi nane hadi 11 tofauti na mbegu nyingine za mgomba zinazotumia miezi 15 hadi 18. Anasema zinavumilia magonjwa kama mnyauko, hazishambuliwi na maradhi lakini pia zikishapandwa zinatoa mbegu kwa wingi.



Gerald Mabuto, akielezea teknolojia ya mbegu za migomba kwa washiriki wanaotembelea banda la Mzumbe. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

Akizungumza na Nipashe kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba jijini Dar es Salaam, Mabuto anasema amefanya utafiti na kuibua mbegu mpya za mgomba ili kumwezesha mkulima kupata mahitaji yake kwa wingi.

Anafafanua kuwa mkoani Kagera na Mbeya wakulima wanalalamika kuhusu upatikanaji wa mbegu bora za migomba.

Anasema mbegu hizo wamezipa virutubisho na madini maalumu ya kutosha yanayofanya ziwe bora zaidi na ukinzani dhidi ya magonjwa yanayoshambulia mgomba.

Mabuto anataja madini hayo kuwa ni pamoja na kalsham na zink ambayo hukuza mmea kwa haraka na kuupa afya bora.

Amezalisha mbegu nne mpya za mgomba za mshare, malindi, kisukari na mkono wa tembo ambazo wakulima wanaweza kuzilima kibiashara na kuongeza kipato.

"Kwa kuanza, tumezisambaza kwa wakulima 15 wa mikoa ya Songwe na Mbeya kwa sababu ndiyo sehemu niliyofanya utafiti. Wamezipenda na ndiyo wateja wetu wakuu hivi sasa kwa ajili ya kilimo cha biashara," anasema.

Anaongeza kuwa chuo kinamsaidia kupata wadau mbalimbali wa kilimo na tayari Wizara ya Kilimo imetambua uzalishaji wa mbegu hizo.

Anakumbusha kuwa Kagera, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga, Morogoro, Kigoma, Mara na Pwani ni mikoa inayolima ndizi kwa wingi na bado zao hili linaendelea kuenea katika mikoa mingine ya Ruvuma, Shinyanga, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam.

Akizungumzia matumizi ya mbegu hizo anasema yanaanza na kuandaa eneo kwa kuchimba mashimo yenye urefu wa futi mbili kwenda chini na upana wa futi mbili pia na kuyajaza mbolea na kumwagia maji yenye kalshamu inayopatikana kwenye mimea ya aloivera.

"Ili kuyapata madini ya kalsham kutoka kwenye aloivera, mkulima anashauriwa kutafuta aloivera kuisaga kwenye blenda au kuiponda kwenye kinu kulingana na mahitaji ya shamba, kisha kutumia juisi iliyosangwa au kuihifadhi sehemu salama."

Baada ya hapo achukue mililita 20 za juisi au maji ya aloivera na kuchanganya kwenye lita 20 za maji kwa ajili ya kumwagilia angalau kwa kila shimo lipate lita moja kwa kila mmea.

**UCHAVUSHAJI**

Mabuto anamshauri mkulima aweke mililita 50 kwenye lita 20 za maji kwa ajili ya kupulizia maua ya mgomba kwa sababu ya kupunguza uharibifu wa bakteria wanaoharibu maua ya ndizi au mgomba.

Anasema utafiti wa mbegu mpya za mgomba ulianza mwaka 2021 hadi 2024 kwa ufadhili wa Chuo Kikuu cha Mzumbe na wakati wa utafiti alikuwa anaangalia uwezekano wa kupata mbegu kwa kutumia muda mfupi na zinazozaa matunda mengi na bora na zenye ukinzani kwa magonjwa.

Anaeleza kuwa bei ya kila mche ni Shilingi 2,000 na zinapatikana chuoni Mzumbe-kampasi ya Mbeya lakini pia mkulima anaweza kupata popote alipo kama akihitaji.

**CHANGAMOTO**

Mabuto anataja uwezeshwaji wa uzalishaji ili kufikia wakulima wengi zaidi pia wengi kutokuelewa na kutambua mbegu hizo.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# ‘Wasioona wanafanya makubwa njooni VETA Dar mjithibitishie’

WATU wanaoishi na ulemavu wanadhihirisha kuwa wana fursa na uwezo wa kufanya mambo ya kujivunia, anasema Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Raphael Mwambalaswa.

Ni miongoni mwa wanafunzi wa Chuo cha VETA Dar es Salaam, anayekamilisha shahada ya uzamivu (PhD), kwenye kutengeneza madirisha ya alminiam.

Kwa juhudi hizo, anapingana na dhana kuwa wenye ulemavu mchango wao ni duni katika uzalishaji na kukuza uchumi, akisema wakipewa nafasi wanafanya makubwa.

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), inawatumia wenye ulemavu, wakijifunza teknolojia tofauti kwenye vyuo vyake.

Kuanzia mwaka 2022/2023 wanafunzi wenye ulemavu waliodahiliwa ni 602 huku waliotoka kwenye mazingira magumu ni 1,712 ambao wanapata mafunzo kama useremala, ujenzi, ushonaji na ufundi simu janja.

Mwambalaswa, asiyeona, anazungumza na Nipashe katika Banda la VETA kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam-Saba Saba, akisema, anafanya utafiti, kupata majibu ya kukabiliana na changamoto kwa wenye ulemavu mfano wasioona.

“Takwimu za ujifunzaji zinabainisha uwezo wa kuelewa kwa asilimia 80 unategemea macho, nikajiuliza kwa namna gani kundi la wasiiona ambao ni watoto watafanya nini ili kufikia asilimia 80 ambayo wao wanaikosa kwa sababu hawaoni ?”

“Nimesoma machapisho na utafiti unaonyesha asilimia 80 ya kujifunza hutegemea macho. Nikaamua kujikita katika eneo hili kwa kuwa na mimi nina ulemavu



Raphael Mwambalaswa. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

wa macho.

“Nikajiuliza changamoto ni zipi kwa watoto wasioona, ambao hushindwa kuifikia asilimia hiyo, wakiwa wanajifunza mfano darasani.”

Anasema anafanya ufundi mwenyewe wa kutengeneza madirisha ya aliminium chuoni VETA, kukamilisha PhD.

Mwalimu wa VETA, Kintu Kiranga, anasema chuo hicho hupokea makundi tofauti ya wanaohitaji kujifunza, ikiwamo watu wenye ulemavu wa aina tofauti.

Anasema Mwambalaswa alifika chuoni hapo, ili kukamilisha PhD kwa kufanya ufundi, kwa kutengeneza madirisha ya alminiam.

“Anaweka vifaa vyake stoo na anajua kipi kinakaa wapi. Anafanya mwenyewe kila kitu kama vile kukata vipande vya madirisha na kuviunda, ni mara chache tutampa msaada.

“Wanafunzi wa aina hii wanatumia uwezo mkubwa wa mguso yaani hisia, akishika kitu fulani anajua ni mashine. Hata katika fedha aliyeona anatumiwa vidole vyake kubaini pesa ina thamani ya Shilingi ngapi,” anasema Kiranga.

Anaongeza kuwa wenye mahitaji maalumu, hasa wasioona ili kumpa mafunzo na aelewe ni lazima kumshikisha kwa mkono, na atakapopapasa ataelewa hii ni nyundo, mashine ya kukata chuma au mbao.

“Muda wa kuwafundisha hadi waive ni mrefu, ili ashike. Hatua ya kwanza inabidi kwenda naye taratibu. Huwezi kuruka hatua ya kwanza hadi inayofuata kama ya awali hajaelewa, ila uwezo wao ni mkubwa sana wakishapapasa kitu kimoja wameshaelewa,” anasema Kiranga.

Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Anthony Kasore, anasema: “Wenye mahitaji maalumu msiwafungie ndani, mlete mtoto, mzee, mama, kijana tumpe mafunzo. Lazima tuwe na taifa lenye ubunifu.”

Anasema VETA pia imekuja na mtaala maalumu kwa ajili ya kuwafunza watumishi wa ndani, mahausi geli ili kumudu kuwahudumia watoto na wazee pamoja na kuwaandaa kufanya kazi nje ya nchi. Kadhalika, inasema inatarajiwa kuongeza idadi ya vituo vya mafunzo kutoka vilivyokuwapo awali 29 mwaka 2020 ili vifikie 143 mwakani, kutokana na kukua kwa mahitaji katika wilaya na mikoa yote nchini.

“VETA tumeleta vitu mbalimbali kuendana na nia ya maonyesho, kama vile huduma tunazotoa katika vyuo vyetu, kama eneo hitaji la mafunzo kwa wanaofanya kazi za ndani, tukiamini mtaala utawasaidiaWatanzania kupata mafunzo kuhudumia watoto, wazee.

“Mtu anafundishwa hadi kupika na tumeona kuna ambao wanahitaji kwenda nje ya nchi kufanya kazi kama hii, ili watambulike kuwa na vyeti tukaona vyema kuwa na ufundi huu ili wawe na ajira inayotambulika,” anabainisha Kasore.

Anaongeza pia kuwa upo mtaala unaotoa mafunzo ya namna ya kutengeneza vifaa tiba, kwa kuanzia mkoani Mara na Geita, huku wakijikita kwa kuwa na mtaala wa watu wanaofanya kazi viwandani kwa kutumia mitambo ya kompyuta.

“Kozi hii imeanza Desemba mwaka jana, hasa kwa ambao wamemaliza vyuo kwa ngazi mbalimbali. Wawekezaji wanakuja nchini sasa hawatapata shida kupata watu wa kusimika mitambo na kuifanyia marekebisho, pia hatujaacha kuwatumia wabunifu,” anaongeza.

Kasore anasema vipo vifaa saidizi kama vya kumenya viazi vya kilo moja kwa dakika, hususan kwa ambao wanakaanga magunia mengi kwenye biashara kila siku, badala ya kupoteza muda kwa kutumia visu.

Anasema wazazi na walezi pamoja na wazee waliostaafu, wafike VETA kujifunza ujuzi aina yeyote, ili kuwafanya wawe na shughuli ya kushughulisha mwili pia na kujiongeza kipato.

Boniface Kiyenze (64), ni mhitimu wa VETA, ameshiriki katika maonyesho ya mwaka huu, akisema kufanya useremala ndiyo maisha yake, akilea familia na wajukuu.

“Nimeajiajiri natengeneza samani. Pale pale ninapoishi Dovya jijini Dar es Salaam, nina sehemu ya kufanya shughuli zangu napata wateja nauza na lea familia. Nina watoto wanne,” anasema.

Kiyenze ana wito kwa jamii isiwatenge watu wa kundi hilo, kwa kuwa wana mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa na kujiinua kiuchumi wao binafsi.

## Mbegu za migomba kwenye paketi zaja, huandaliwa kutoka kwenye ndizi mbivu

INATOKA UK.11

Kilimo cha migomba ni maarufu hapa nchini kwa sababu ndizi zinatumika kwa chakula kwa baadhi ya mikoa mfano, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya na Kigoma hivyo ni zao muhimu kwa wananchi na wafanyabiashara pia.

Anasema ndizi ni moja kati ya mazao ya biashara iwapo wakulima watapata mbegu bora na kufuata kanuni endelevu za kilimo kama kupanda aina bora ya migomba inayozaa mazao na kukubalika katika masoko ya kimataifa.

Migomba inayolimwa Tanzania kwa mujibu wa Wizara ya Kilimo, asili yake ni India na Malaysia, iliyofika Afrika Mashariki katika karne ya tano.

Baadhi ya faida nyingi za ndizi ni chakula zikiliwa mbivu, ni matunda, ni mlo kamili zikipikwa na nyama, samaki na maharage.

Kadhalika ni maarufu kwenye vitafunwa hukaangwa, kuchomwa, kutengenezwa viwanda ambao ni mkate wa ndizi na pia hutengenezwa krips.

Ni malighafi kuzalisha bidhaa nyingine kama pombe, juisi, chakula cha mifugo, hutengenezwa unga, mbolea (mboji), majani na maganda yake ni matandazo shambani (mulch), majani yake huezekea, migomba hutoa kivuli na kuleta ubaridi nyumbani.

Aidha, hutoa nyuzi za kutengenezea bidhaa za sanaa, majani ni miamvuli wakati wa mvua vijijini na sahani za kulia hasa Kagera, pia hutengenezwa kama vikombe kunywea vitu mbalimbali.

Ni kata ya kubebea mizigo kichwani, ni maganda yake ni bomba za kusafirisha maji mtoni au kisimani kuyasambaza vijijini.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

DIRA 2050

# Wanawake wakataa kupewa 'lifti', usawa kijinsia uwe taa kuiongoza nchi

• Yajayo kila kitu ni 50/50 wasisikie vifo vya wazazi

KATIKA kongamano la kutoa maoni ya kuandaa dira ya maendeleo ya taifa 2050, wanawake kwa sauti moja, wanasema hawako tayari kupewa 'lifti' au kuwekwa pembeni kwenye masuala ya maendeleo ya nchi kama ilivyotokea kwenye dira 2025 inayomalizika.

Wakirejea takwimu za sensa ya mwaka 2022 kuwa idadi yao ni zaidi ya asilimia 51 au nusu ya Watanzania, wanataka usawa wa kijinsia uwe taa inayoliongoza taifa dira mpya 2050.

Wanataka usawa uonekane katika kila sekta kuanzia uchumi, jamii, siasa, uongozi, umiliki rasilimali na popote yanapofanyika maamuzi.

Wanataka ifikapo 2050 nafasi zote za uongozi na maamuzi ziwe na uwakilishi wa 50/50, anasema Anna Kulaya Mratibu wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), anayewasilisha maoni ya wanawake.

Anayasema kwenye kongamano la kitaifa la wanawake kuchangia maoni ya dira ya taifa 2050, akisema wakati umefika wa kurekebisha upungufu wa dira inayopita iliyokuwa na mapengo mengi ya kukosekana usawa kijinsia yaliyorudisha nyuma na kuumiza zaidi wanawake na makundi ya wanyonge.

Kongamano hilo likiandaliwa na Mfuko wa Udhamini wa Wanawake (WFT), Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na WiLDAF pamoja na wadau wengine, likifanyika Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, kutoa moani kwa Tume ya Mipango na Uratibu wa Dira ya Taifa 2050.

Kadhalika wanawake wanataka dira mpya itakayokomeshwa vifo vinavyohusiana na uzazi na kwamba mwanamke anayezaa nguvu kazi, wapigakura, walipa kodi na viongozi asipoteze maisha kwa sababu yoyote ile na pia mtoto anayezaliwa aishi.

Ni katika eneo la afya Anna anaposema, "Tunajua wanawake ndio wazazi wanaoleta nguvu kazi ya taifa na ili taifa liendelee linahitaji watu, tunataka dira ya 2050 kusiwe na kifo hata kimoja kwa sababu yoyote ile."

Wanataka huduma za afya za msingi kwa kila mtu kwa ubora tena zinazopatikana kwa ubora na gharama nafuu, huku kila Mtanzania akimudu bima ya afya yenye ubora kuendana na hali ya maisha.

Aidha, Anna anasema wanawake wanataka kusiwe na mtoto anayekufa kutokana na ukosefu wa huduma ya afya, lishe bora na ulinzi dhidi ya ukatili na udhalilishaji.

Pamoja na hayo vitendo vyote vya ukatili pamoja na rushwa ya ngono, udhalilishaji kijinsia, kiuchumi na kimwili vinavyokwamisha wanawake viwe historia ndani ya dira 2050.




Wakurugenzi TGNP, Lilian Liundi na Rose Marando wa Mfuko wa Kuwezesha Wanawake (aliyesimama), wakishiriki kongamano la wanawake na maoni ya dira 2050. **PICHA: MWANDISHI WETU**

### MAISHA BORA

Akizungumzia kuishi kwa viwango anasema wanataka kuwe na maisha bora na mazuri ifikapo 2050 tena kusiwe na kaya isiyo na chakula chenye bora na kusiwe na Mtanzania mwenye ukosefu wa chakula bora na cha kutosha.

Kadhalika kwenye elimu wanataka ijenge misingi ya uwajibikaji kulinda rasilimali za nchi na kukomesha wizi, ubadhirifu wa mali za umma.

Pia, elimu iwawezeshe wanawake kusoma kuelimika na kuwa majasiri kudai na kutetea haki zao, kutumia vipaji na kujisimamia kama raia huru na kusiwe na ubaguzi wowote wa kijinsia.

Aidha, wanawake wanataka taulo za kike zipatikane kwa kila binti shuleni, tena shule ziwe salama na bora kwa mwanafunzi yeyote kuanzia msingi hadi vyuo elimu ya juu.

Kwa upande wa ndoa zisizokubalika utotoni, wanawake wanataka kusiwe na kuolewa chini ya miaka 18 na hukumu ya mahakama ya kurekebisha sheria ya ndoa itekelezwe lakini pia mimba za utotoni zisisikie popote.

Wanawake wana maoni sekta ya maji wakisema 2050 kila kaya iwe na maji safi na salama, tena taifa kwa gharama yoyote lilinde vyanzo vyote vya maji popote vilipo.

### UMASKINI USISIKIKE

Akiwasilisha maoni eneo hili mratibu WILDAF anasema: "Tanzania ina rasilimali nyingi mno zitumike kwa umakini na uwajibikaji kwa kuzingatia usawa kijinsia, umaskini na ufukara viwe historia. Wanawake tunadai ifikapo 2050 utajiri wa Tanzania utumike kwa manufaa ya kila mmoja wanawake kwa wanaume."

Aidha, wanataka uwekezaji kwenye vipaumbele vya taifa uondoe pengo la ajira, ujira kiduchu na umaskini unaoonekana kwa wanawake, ukivikwa sura ya mwanamke wa kijijini asiye na chakula bora, hamiliki ardhi, mwenye maisha duni, anayekandamizwa na mfumo dume, anayeumizwa na ukatili wa kijinsia, rushwa ya ngono, asiye na barabara bora na zaidi hana mtaji wa kuanzisha biashara.

### AMANI UTULIVU

Ujumbe wao ukawa huu: "Hatuwezi kuwa na Tanzania yenye amani na utulivu kama wanawake, wasichana, watoto, wenye mahitaji, wanaoishi na ulemavu wananyanyaswa na kudhalilishwa kimwili, kingono, kisaikolojia na kiuchumi."

Wakataka vyombo vya dola vinavyosimamia ulinzi viwajibike kwa raia wote kuanzia kwenye kaya, jamii, shuleni na kazini kukomesha ukatili na udhalilishaji na kwamba ukatili wa aina yoyote kwa wanawake, watoto na watoto wa kiume utokomezwe.

Ifikapo 2050 wanawake wanataka kusisikike taarifa za vifo vya wenye ualbino, kuuza viungo vyao, watoto wenye ulemavu kufungiwa ndani, wanawake wazee kuuliwa kwa madai ya uchawi na pia watoto kunajisiwa.

### USHINDANI KIUCHUMI

Wanawake wanaieleza tume ya dira kuwa vikwazo vya kiuchumi pamoja na mabadiliko ya tabianchi vimeongeza mzigo wa umaskini kwa wanawake.

Wanataka ifikapo 2050, mfumo wa uchumi uwe jumuishi na kuendeshwa na sera na sheria zinazowanufaisha wanawake, watumie fursa za kibiashara, uwekezaji, huduma za fedha na matumizi ya teknolojia yenye tija.

Wanadai uwekezaji kwenye maeneo yanayotoa ajira kwa wanawake, kama kilimo, afya, elimu lakini pia sekta za kipaumbele kukuza uchumi kama migodi, utalii, barabara na ujenzi ziwe na mikakati mahususi ya kupanua ushiriki wa wanawake kwenye ajira.

Akichambua mapengo ya dira inayomalizika, Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi, anasema ilikuwa na upungufu mkubwa na haikuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia na kwamba ni lazima usawa uzingatiwe ili kila kinachotekelezwa kinufaishe kila Mtanzania.

Anatolea mfano suala la kuwa na Tanzania yenye amani na utulivu, kwamba halina mantiki kama wanawake na wasichana na makundi na wanyonge wanateseka na ukatili wa kijinsia.

Akizungumzia vipengele vya maendeleo endelevu, maadili mema, uadilifu na kuthamini utawala wa kisheria na kupinga rushwa, anasema kulikuwa na udhaifu na kukosekana uwajibikaji wa kujali masuala ya kijinsia.

"Suala la rushwa halikupambanua rushwa ya ngono ambayo ni gonjwa linalotafuna taifa ipo kila mahali. Ili kuchota maji unatoa rushwa ya ngono kwa sababu yanauzwa au kwenye kuni ni lazima utoe ngono ili uingie msituni kupata kuni ni tatizo."

Akichambua kipengele cha elimu na kuwa na jamii iliyoelimika, inayojifunza zaidi na kuwa na taifa lenye fikra na ujasiri linaloishi kwenye dunia yenye ushindani, anasema dira inayomalizika haikuakisi uhalisia wa maono hayo kwa sababu ya kukosekana usawa kijinsia.

"Unapozungumzia ushindani, hivi mwanamke au msichana unashindaje umebeba ukatili kijinsia, unafanyakazi zisizolipwa, huna ardhi wala hupati mkopo unategemea kausha damu na vijisenti vichache vya mkopo wa asilimia 10 wa halmashauri.

Tujiulize unashindanaje?" anahoji Lilian Anakumbusha kuwa taifa haliwezi kuwa na maendeleo endelevu iwapo nusu ya raia wake ambao ni wanawake wameachwa kwenye kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo.

ELIMU

NA SHABAN NJIA, KAHAMA

# Ushuhuda wanaoozwa utotoni wanavyoteswa

NDOA na mimba za utotoni zinaacha kovu zisizofutika kwa mabinti waathirika, akiwamo Queen Maige wa Butiama mkoani Mara, anayeeleza jinsi alivyoozwa utotoni kwa shinikizo la mjomba, na leo ni mtumwa wa kupigwa na mume kila wakati.

Queen anadai, mjomba wake alimhadaa mama yake (majina yanahifadhiwa), akimshinikiza aruhusu Queen aolewe kwa mahari ya ngombe sita, ambayo mama yake hakuambulia chochote.

Anaongeza kuwa ndoa hizo ni vikwazo kwa wasichana kupata elimu na kutimiza malengo yao kitaaluma kwa sababu, wanaishia kuteseka na kukwama kimaisha.

Anasema wanalazimishwa kuingia kwenye ndoa na wazazi au walezi bila kujali kuwa wako shuleni au kiumri ni watoto, madai yao ni kuzipatia familia mali kutoka kwenye mahari na mifugo ili kupunguza umaskini.

Ni mikasa inayotokea vijijini zaidi kuliko mijini huko wanafunzi wasichana wanabadilishwa na ng'ombe na mahari ili familia zipate ahueni.

Kwa mujibu wa ripoti ya haki za binadamu inayotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ya mwaka 2023 Tanzania Bara, matukio 2,953 ya mimba za utotoni yaliripotiwa.

Ni katika mikoa mbalimbali, waathirika wengi wakiwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari vijijini, wanaolazimishwa kufanya vibaya kwenye masomo ili wafeli mitihani kwa lengo la kuozwa.

Mila zenye madhara na umaskini ni miongoni mwa vichocheo vikubwa vya ndoa na mimba za utotoni kwa mujibu wa ripoti.

Kadhalika LHRC inasema si mimba pekee wapo walioambukizwa magonjwa ya ngono kama UKIMWI na kwamba waathirika wengi wanatoka katika familia maskini.

Shirika la kiraia la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), linanyoosha mkono kusaidia mabinti wanaoathirika na kuozwa utotoni.

Ni kupitia mradi wa chaguo langu haki yangu, unaowakutanisha mabinti wenye umri wa miaka 10 hadi 24 wa mikoa ya Shinyanga na Mara, kuwapatia ujuzi kwenye vyuo vya ufundi ili wajifunze stadi za maisha zinazowainua kiuchumi.




Mnufaika Elizabeth Mussa (19) wa Kishapu-Shinyanga, akionyesha ujuzi wa chereheni. **PICHA: SHABAN NJIA**

> Haikuwa rahisi kulikubali hilo na kila siku nilipigwa ili nikubali kwa shinikizo la kupata fedha kuisaidia familia iondokane na ugumu wa maisha waliokuwa nao.

Kupitia mradi huo wengi wamepaza sauti na kueleza yaliyowapata na kukatisha ndoto za masomo walipolazimishwa kuolewa na familia zao, kubeba mimba na kufukuzwa nyumbani, kuogesha dawa za mvutano wa mapenzi ili aolewe haraka na kubakwa pasipo watuhumiwa kushtakiwa.

### SAUTI ZA WASICHANA

Nipashe inakirejelea kisa cha Queen Maige (21), aliyelazimishwa kuolewa na mjomba wake akiwa na miaka 15, ili afaidi mahari ya ng'ombe sita, alizodai alijichukulia mwenyewe bila kushirikisha wanafamilia.

"Haikuwa rahisi kulikubali hilo na kila siku nilipigwa ili nikubali kwa shinikizo la kupata fedha kuisaidia familia iondokane na ugumu wa maisha waliokuwa nao."

Anasema, aliolewa baada ya kumaliza la saba lakini hakufurahia ndoa kwasababu kila siku mumewe alikuwa akimpiga bila huruma.

Queen anasema, akiwa darasa la saba mwaka 2015 katika Shule ya Msingi Kinyalili huko Butiama alianza kusikia mjomba wake, akimlazimisha mama yake kukubali aolewe.

"Mwaka 2016 niliolewa kwa ng'ombe sita ambazo pia sijui zimeelekea wapi kwasababu mama yangu hakupewa hata mmoja," anasema kwa uchungu.

"Leo naumwa sana kifuani, ni baada ya mume wangu kunipiga teke bila sababu haya yote yametokea baada ya baba yangu kufariki tukabaki na mama na wajomba. Nimekuwa mama wa watoto wawili. Niwaombe wale wenye wazazi wanaojua umuhimu wa elimu wawasaidie watoto wasome kwa bidii na mabinti kupenda elimu," anashauri Queen.

Anasema yote hayo ni matokeo ya tamaa za mjomba wake ambayo ilimpeleka hadi kumlaghai mama yake ili aruhusu aolewe na sasa wote tunahangaika.

Queen ni miongoni mwa wasichana wanaosaidiwa na WiLDAF kupata ujuzi wa ufundi cherehani ili aweze kulea watoto wake wawili, mama yake na wadogo zake watatu.

Mnufaika mwingine wa ujuzi unaotolewa na WILDAF ni Mbula Mussa, kutoka Kata ya Mondo Wilaya ya Kishapu, anayesema, baada ya kuhitimu elimu ya msingi, aliozwa, hata hivyo ameachana na mume kutokana na kupigwa kila uchao.

### LENGO WiLDAF

Mratibu wa mradi wa chaguo langu haki yangu kutoka WiLDAF, Joyce Kessy, anasema shirika linawaibua mabinti wenye umri wa miaka 10 mpaka 24 na kugharamia mafunzo ya ufundi ili wapate ujuzi mbalimbali na kujiinua kichumi.

Anasema, mwaka huu wamewafadhili mabinti 164 waliokatisha masomo kwa sababu ya ndoa ya utotoni, mazingira magumu, mimba na kukeketwa kupata ujuzi.

Joyce anasema kati ya hao 45 wanatoka mkoa wa Mara, wengine 75 ni kutoka Kishapu, 44 Kahama mkoani Shinyanga.

Anawataka kuchangamkia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri ili kupata mitaji na gharama za kuendesha miradi watakazofungua.

Joyce anasema, tangu mwaka 2022 mpaka sasa wamewafikia mabinti zaidi ya 1,500 wenye umri huo na kuwapatia elimu ya afya ya uzazi, madhara ya mimba na ndoa za utotoni kwa lengo la kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwenye familia wanazotoka.

Swahiba Chemchem, Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Kahama anasema, mabinti wengi wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na wanafamilia kwa kulazimishwa kuolewa wakiwa wadogo au kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya mwisho ili wasifaulu.

Anasema, vitendo hivyo vimekuwa vikichangia mabinti wengi kushindwa kutimiza ndoto zao za kimasomo na sasa wanalazimika kutembelea kaya na kuzielemisha umuhimu wa elimu hasa zile zinazoishi pembezoni na wale wanaokiuka sheria wamekuwa wakifikisha mahakamani.

Swahiba anasema, mabinti hao waliohitimu mafunzo watawaunganisha kwenye vikundi vya ujasiriamali kwa lengo la kupata mikopo ya asilimia 10 isiyokuwa na riba ili wapate mitaji ya kujiendeleza kupitia kile walichojifunza na kuwasimamia ili wasije kuuza vifaa vya kazi watakavyokuwa wapewe.

Katibu wa umoja wa vyuo vya ufundi Kanda ya Magharibi, Thomas Batenga, anapongeza juhudi za WiLDAF na mashirika mengi yanayofanya kazi za namna hii ya kusaidia makundi hayo na kuhakikisha yanatimiza ndoto zake kwa hatua nyingine na kuwaondoa kwenye utegemezi na kutoingia kwenye makundi maovu.

Anasema, wale wanaojifunza ufundi wa umeme pamoja na bomba wasiishie kusaidiwa kupata vifaa vya kazi na badala yake wawakatie pia na leseni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) wanaobainika kufanyakazi bila kuwa na leseni kuwaepusha na faini ya Shilingi milioni 10 au kwenda jela miaka mitatu au vyote kwa pamoja.



## ‘Bosi’ Wizara ya Fedha aving’ata sikio vikundi vya kijamii

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, amevishauri vikundi vya kijamii nchini kuanzisha miradi ya maendeleo ili kusaidia kukuza uchumi wa taifa.

Omolo alitoa ushauri huo wakati akizindua kikundi cha wanawake wafanyakazi wa wizara hiyo kijulikanacho kwa jina la Golden Women Gala uliofanyika mwisho wa wiki jijini hapa.

Alisema vikundi hivyo vya kijamii vinaweza kuanzisha miradi ya maendeleo ili kusaidia kukuza uchumi wa taifa.

Omolo alisema vikundi vingi vimekuwa vikiishia kusaidiana wakati wa matatizo, lakini wanauwezo wa kuanzisha miradi ya maendeleo.

Kadhalika, alisema vikundi hivyo vinatakiwa kuwa na uendelevu kwa kutengeneza Katiba zenye malengo ya muda mrefu.

Aidha, aliwataka wafanyakazi hao wanawake katika wizara hiyo kufanya kazi kwa kujiamini na kuacha kutegemea watu wa kuwabeba.

Kadhalika, aliwataka kufanya kazi kwa uwezo wao na kujiamini pamoja na kushirikiana katika mahali pakazi.

Mwenyekiti wa Golden Women Gala Wizara ya Fedha, Consolata Maimu, alisema kikundi hicho kinaundwa na wanawake wafanyakazi wa wizara waliopo na waliohama na kilianzishwa mwaka 2023 kikiwa na wanachama 247 na hadi sasa wapo 288.

Maimu alisema malengo ya umoja huo ni kusaidiana katika shida mbalimbali ikiwemo misiba, ugonjwa na sherehe.

Aliongeza kuwa pia umoja huo unasaidia kwa kuwajengea stadi za maisha, ujasiriamali na kufahamiana katika eneo lao la kazi.

Naye mtoa mada katika uzinduzi huo, Dk. Japhet Swai kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe aliwataka wananchi kuwatumia wataalamu wa saikolojia na madaktari wa hospitali hiyo ili kupata ushauri wa kitaalamu kuhusu afya ya akili.

Dk. Swai alisema magonjwa ya akili yanasababishwa na matatizo mbalimbali katika jamii yakiwamo ya familia.

Alisema kuna baadhi ya magonjwa ya akili ni ya kurithi na mengine yanasababisha sononа na msongo wa mawazo na kuathiri maendeleo ya mtu katika ufanisi wa kazi, hivyo yanatakiwa kuzuiliwa.

Hata hivyo, alisema tiba pekee ya magonjwa hayo ni ushauri kutoka kwa wataalamu na kutumia dawa kwa ushauri wa madaktari wenye taalamu hiyo.

# Afariki dunia kwa kukanyagwa na lori

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKAZI wa Mtaa wa Sabasaba Manispaa ya Singida, Rehema Omari, amefariki dunia baada ya kugongwa na lori la mizigo baada ya kuanguka kutoka kwenye pikipiki.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa ajali hiyo imetokea juzi majira ya saa 7:00 mchana eneo la karibu na Rafiki Resort, Barabara ya Singida-Mwanza.

Alisema mwanamke huyo alianguka kutoka katika pikipiki aliyokuwa amepakizwa baada ya dereva wa pikipiki kuyapita magari mengine eneo ambalo sio upande unaostahili na kukutana na matuta.

Alisema hivyo mwanamke huyo alianguka katikati ya barabara ambapo lori lililokuwa nyuma likamgonga kwa kumkanyaga kichwani na kusababisha umauti wake.

Kamanda Kakwale alisema baada ya tukio hilo lori lililomgonga halikusimama na pia pikipiki iliyokuwa imembeba ilikimbia na kutokomea kusikojulikana na Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka dereva huyo.

Hivyo, aliwataka madereva hususani wa pikipiki na bajaji kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizokuwa za lazima.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Sabasaba, Juma Abdallah, ambaye alifika eneo la tukio alisema marehemu alianguka katika pikipiki kutokana na kukaa mkao wa pembeni ambao wanawake wengi wanapenda kukaa wakiwa kwenye usafiri wa pikipiki.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, akizungumza wakati wa kuzindua umoja wa wanawake wafanyakazi wa wizara hiyo, ujulikanao Golden Women Gala katika hafla iliyofanyika mwishoni wa wiki jijini Dodoma . **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yashauriwa kulishirikisha Bunge kabla ya kukopa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kutumia kamati za Bunge zinazohusika na masuala ya fedha kabla ya kuingia kwenye mikopo, ili kupata ushauri utakaosaidia fedha hizo kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo badala ya kwenda mifukoni mwa watu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Madeni na Maendeleo Tanzania (TCDD), Hebron Mwakagenda, alisema hayo juzi jijni hapa kwenye warsha iliyowakutanisha vijana kutoka vyuo vikuu na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, kwa ajili ya kujifunza jinsi ya kufuatilia matumizi ya fedha za mikopo kutoka nchi za nje.

Alisema ni vyema serikali inapotaka kukopa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka nchi za nje ikapitia katika kamati za Bunge zinazohusika na masuala ya fedha, ili kupata ushauri na kujiridhisha kama kweli kiasi kinachokopwa kitakwenda kwenye miradi inayokusudiwa.

Alisema licha ya kuwa siyo vibaya nchi kukopa fedha kutoka nchi za nje kwa ajili ya maendeleo lakini ni vyema Waziri wa Fedha akashirikisha kamati za masuala ya fedha kwa lengo la kupata ushauri zaidi wa namna bora fedha hizo zitakavyoweza kutekeleza miradi hiyo na namna bora ya kurejesha deni.

Alisema deni linaweza kuwa zuri kwa maendeleo lakini kama halitakuwa katika uratibu mzuri inaweza kuwa mwiba kwa vizazi vijavyo vya Watanzania.

Pia alisema Watanzania ndiyo watahusika kwa njia moja au nyngine katika kulipa deni, hivyo ni wajibu wao kuhakikisha wanakuwa na ufahamu na uelewa mzuri jùu ya matumizi bora ya fedha za mikopo ya maendeleo kutoka nje ya nchi.

Naye Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Canon Moses Matonya, akifungua warsha hiyo aliwataka vijana kuwa wafuatiliaji wa karibu katika kutambua kama fedha za mikopo ya maendeleo zinatumika vyema au vinginevyo.

Alisema: “Pamoja na kufuatilia matumizi ya fedha za mikopo ya maendeleo lakini pia vijana wanatakiwa kutokuwa waoga pale wanapoona matumizi yaliyokusudiwa hayafanyiki na badala yake wanatakiwa kuhoji kwa fedha za madeni kutoka nchi za nje yatalipwa na Watanzania wenyewe kwa vizazi na vizazi”.





# Wanakijiji 3,000 wakatiwa bima ya afya

● Ni baada ya fidia ya mradi wa Liganga, Mchuchuma kuzaa faida

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

SERIKALI ya Kijiji cha Mundindi wilayani hapa Mkoa wa Njombe, imewalipia bima ya afya wakazi 3,149 baada ya kupokea faida ya gawio la mwaka la Shilingi milioni 41 kutokana na uwekezaji kwenye moja ya taasisi za fedha.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mwenyekiti wa kijiji hicho, Sapi Mlelwa, wakati wa kukabidhi bima hizo kwa wakazi hao ikiwa ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na kijiji chao.

Mlelwa, alisema fedha hizo ni kutoka kwenye hati fungani ya shilingi milioni 400 walizoziweka baada ya kupata fidia ya shilingi milioni 464 ili kupisha mradi pacha wa chuma cha Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma.

Alisema gawio hilo la kwanza waliona ni vyema kuwakatia wanakijiji wote bima ya afya ambayo imegharimu Shilingi milioni 12,930,000.

"Serikali ya kijiji, kata na ngazi zote tuliona kuna haja wananchi kunufaika moja kwa moja kwa fedha hizi kwa kuwakatia bima ya afya kwa kuwa kuna baadhi wamekuwa wakishindwa kumudu gharama za matibabu," alisema Mlelwa.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema kijiji hicho ni cha mfano nchi nzima kwa kiongozi wake kufanya ubunifu huo mkubwa.

Mtaka alimwagiza Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Stanley Mlay kuhakikisha kituo cha afya cha kata hiyo kinakuwa na dawa za kutosha ili wananchi wapate dawa kulingana na ugonjwa walionao.

"Mganga Mkuu fedha hizi zilizolipwa na kijiji hiki ni fedha nyingi na zinazojitosheleza kununua dawa za aina zote, sasa sitegemei kusikia wanakijiji hawa wanaishia kupewa Panadol tuu badala ya dawa ya ugonjwa husika aliokutwa nao," alisema Mtaka.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema anaona fahari sana fedha za fidia zimeweza kuleta manufaa makubwa kwa wananchi hao na kuahidi kwenda kuisisitiza serikali katika upatikanaji wa dawa za uhakika katika hospitali na vituo vyote vya afya jimboni mwake.

"Kwa sasa sina hofu na utoaji huduma katika kata hii, maana najua mna kituo cha afya kikubwa, chenye vifaa tiba vya uhakika na gari ya kubebea wagonjwa, ni matumaini yangu kila kitu kitaenda sawa," alisema Kamonga.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, alisisitiza kuwa fedha zinazoendelea kupatikana zitasaidia vijana kupata elimu ya ufundi itakayo wawezesha kupata ajira katika miradi wa Liganga na Mchuchuma.

Diwani wa Kata ya Mundindi, Wise Mgina, alisema suala la kusomesha vijana lipo katika mpango mkakati ili kukabiliana na tatizo la ajira katika wilaya hiyo.

"Tumelenga kuwainua watoto waishio katika mazingira magumu na yatima kwa kuwasomesha kozi fupi katika vyuo vya ufundi VETA (Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi)," alisema Mgina.



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Benki ya Azania, Augustino Matutu, alipotembelea banda la benki hiyo kwenye maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Wazazi kitaifa mkoani Katavi jana. Kulia ni Meneja wa Benki ya Azania tawi la Tunduma, Mulaga Sunday na kushoto ni Meneja Masoko, Allan Msalilwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wa dini wafanya maombi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

VIONGOZI wa dini mkoani Mbeya, wameanza kutekeleza ombi la Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera la kufanya maombi maalumu kwenye maeneo ambayo kunatokea ajali za mara kwa mara kwa kutembelea eneo la Mbembela ilipotokea ajali hivi karibuni na kuua watu 17.

Jukwaa la Wakristo wa madhehebu mbalimbali jijini Mbeya, walifanya maandamano ya amani mwishoni mwa wiki iliyopita kutoka Kanisa la Moraviani Jimbo la Kusini Magharibi Usharika wa Iyunga mpaka Mbembela.

Walipofika katika eneo hilo, walifanya maombi maalumu ya pamoja kuzuia ajali ambazo zimekuwa zikitokea na kugharimu maisha ya watu, kuwaacha wengine na ulemavu wa kudumu na uharibifu wa mali.

Askofu wa Kanisa la Moraviani Kusini Magharibi, Robert Pangani aliwataka wananchi kuendelea kudumisha amani na upendo ili taifa liendelee kustawi.

Askofu Pangani, alisema katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi Mkuu wa mwakani ni lazima kila Mtanzania ashiriki kuzuia matukio ya uvunjifu wa amani.

"Tumekuja kufanya maombi haya katika eneo hili kwa sababu ndilo lililobaki ambalo ajali zimekuwa zikitokea mara kwa mara, lakini tunapofanya maombi haya hatuombi kwa ajili ya hapa tu, tunaombea taifa zima," alisema.

Alisema kwa muda mrefu Tanzania imekuwa ikisifiwa kuwa taifa lenye amani zaidi na hivyo akasisitiza kwamba kila mmoja anatakiwa kuendelea kulinda heshima hiyo.

# Mamalishe, babalishe washauriwa kuzingatia usafi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMALISHE na babalishe jijini hapa, wameshauriwa kuzingatia usalama wa afya za wateja wao wakati wa kuandaa chakula kwa kusafisha vyombo na matunda.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Mohamed Aziz, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa uzinduzi wa karo la kuoshea vyombo na matunda katika Soko la Sido miongoni mwa masoko makubwa ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Karo hilo limejengwa na shirika lisilokuwa la serikali la HELVETAS kupitia mradi wa Kuboresha Mifumo ya Chakula katika majiji (IC4N) ambao ni miongoni mwa miradi ya ushirikiano kati ya Jiji la Mbeya na Jiji la Zurich la nchini Uswis.

Aziz aliwataka kuhakikisha wanalitumia karo hilo kusafisha vyombo na matunda ili kuwaepusha wateja wao kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kwa kula uchafu.

Alisema endapo hawatalitumia karo hilo, wafadhili hawataona umuhimu wa kufadhili mradi huo.

"Mtu akiwa anaandaa chakula kwenye maeneo ambayo ni machafu lakini unakuta wateja wanamiminika ndio tetesi za ushirikina zinaanza, mambo kama haya huwa hayafai kabisa kwa hiyo nawaomba sana mjitahidi kuzingatia usafi," alisema Aziz.

Meneja wa Mradi wa Kuboresha Mifumo ya Chakula wa HELVETAS, Agnes Mahembe, alisema ujenzi wa karo hilo na kuweka mifumo ya maji umegharimu Sh. milioni 13.

Agnes alisema wamejenga karo hilo kutokana na maombi ya wajasiriamali wa eneo hilo.

Alisema katika mradi huo wamejenga karo, kuziba mitaro ya maji machafu inayopita kwenye eneo la kuandalia chakula na kuezeka sehemu ya kuandalia chakula.

Ofisa Uhusiano wa Ushirikiano kati ya Jiji la Mbeya na Zurich, Ally Nnunduma, alisema mradi huo ni muhimu kwa mamalishe na babalishe ili kulinda afya za wateja wao na wananchi wengine.

Alisema kwenye kikao cha viongozi wa majiji hayo kilichofanyika Zurich Machi Mwaka huu, viongozi wa Jiji la Zurich waliahidi kuongeza ushirikiano kwa kuboresha miundombinu ya mifumo ya chakula.

Baadhi ya mamalishe hao walilishukuru shirika hilo kwa kuwasaidia kuboresha mazingira ya kazi yao na kuwaomba wawawekee taa ili waweze kutoa huduma kwa wateja wao wakati wa giza.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Hadija Saliba, alisema kabla ya kuboreshewa eneo hilo walikuwa wanapata shida wakati wa jua kali na mvua, lakini shirika hilo limewezekea na kuwavutia wateja.

Vilevile alisema kabla ya mradi huo walikuwa wanalazimika kwenda kutafuta maji lakini kwa sasa huduma hiyo wanaipata jirani baada ya kusogezewa na shirika hilo.



# SMZ yaendelea kuimarisha utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inaendelea kuimarisha miundombinu na fursa za biashara kwa wananchi kupitia sekta ya utalii visiwani hapo, imeelezwa.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Aboud Suleiman Jumbe, katika kikao cha kuwasilisha tathmini za awali za kuchakata maoni ya wadau wa utalii na wananchi wanaonufaika na mradi wa kuendeleza utalii wa vijiji vya Nungwi, Chwaka na Makunduchi.

Jumbe, alisema mradi huo unaotekelezwa na mradi wa kuimarisha uchumi jumuishi Zanzibar (BIGZ) chini ya udhamini wa Benki ya Dunia (WB), utatoa fursa kwa wananchi kwa biashara zao kuwa bora kupitia utalii na kufanikisha kile ambacho serikali imekikusudia.

Alisema mradi huo shabaha yake ni kuwanufaisha wananchi katika dhana ya utalii kwa wote ili kuimarisha miundombinu na kufungua fursa zaidi.

Vilevile, alisema mradi huo utawasaidia wananchi kupata maendeleo ya haraka.

Mshauri wa Mambo ya Ushirikishwaji Jamii katika mradi ya shirika linalohusika na usanifu wa Miradi ya (BIG -Z) kutoka Italia, Manjoro Kambili, alisema wapo katika hatua ya utoaji wa taarifa katika maeneo ya mradi huo.

Kambili, alisema kipaumbele chao ni kuona miradi iliyopo inawanufaisha wananchi kwa kuondokana na umaskini uliokithiri miongoni mwao.

Alisema pamoja na kuwepo kwa miradi mingi ya uwekezaji, jamii inakosa kupata fursa za utalii kwa kujiona wageni kwa uwekezaji katika sekta hiyo.

Hata hivyo, alisema katika taarifa yao ya awali mambo waliyoyaangalia ni miundombinu kwa maeneo yenye utalii, maisha ya kila siku ya wananchi, mazingira, utalii, fursa na changamoto.

Alisema wakati wanafanya tathmini waliona ushiriki mzuri wa wananchi na utayari wao kwa kutoa ushirikiano kwa hali na mali.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akiwa Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Seif Abdalla Juma, akimwelezea kuhusu miradi inayojengwa na mamlaka hiyo, wakati wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumo kupunguza matumizi kwa taifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Mzee Suleiman Mdewa, amesema mfumo wa kidigitali wa mali za serikali ni muhimu katika uchumi kwa sababu utalipunguzia taifa gharama.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo kwa watendaji wa serikali wakiwamo wahasibu na maofisa wa teknolojia ya mawasiliano ambayo yameandaliwa na ofisi ya mkaguzi mkuu wa mali za serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la UN.

Alisema mfumo mzuri wa kujua mali utaiwezesha serikali kupanga mipango yake mizuri na kudhibiti mianya ya wizi kwa mali za serikali.

"Ukiwa na mfumo mzuri wa kujua mali zako utajua kiasi gani unaweza kutumia kutengeneza gari yako ambayo pengine imeharibika, lakini ukiwa huna mfumo wa kuelewa mali zao zitaibiwa bila ya kujua," alisema.

Alisema mfumo huo utaweka udhibiti wa upotevu na wizi wa mali za serikali.

Wahidi Sanya, Msajili wa Hazina, alisema watendaji hao wanapatiwa mafunzo kuhusu mfumo huo ili kutambua jinsi ya kuingiza data na mambo mengine yatakayosaidia katika manunuzi.

"Jambo jipya hasa kama hili la mifumo huchukua muda kidogo, lakini tushaanza kuona matokeo yake tangu kuanza kwa huu mfumo na ni mfumo rafiki hivyo watumiaji wanaanza kufahamu na kuutumia," alisema Sanya.

Mshiriki wa mafunzo hayo, Ahmed Talib kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, alisema matarajio yao yatafunguwa nafasi kwa taasisi za serikali katika kuboresha uhifadhi wa mali za serikali na kupata uelewa wa kuhifadhi mali hizo na kupunguza gharama za matumizi katika mali za serikali.

"Mafunzo haya pia yatatanua wigo kwa watendaji wa serikali katika kusimamia mali za serikali na kupitia mafunzo haya tutaiwezesha serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuletamaendeleo kwa Zanzibar, alisema.

Ofisa kutoka UN ambaye anaratibu mafunzo hayo, Daniel Tlatz, alisema yatasaidia serikali kuweka kumbukumbu za mali na matumizi sahihi.

# Wakulima wahamasishwa kuongeza uzalishaji mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKULIMA wa mwani wametakiwa kuongeza uzalishaji ili kuongeza ubora na kukabiliana na ushindani katika soko la nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari Ofisini kwake Malindi mjini Unguja, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mwani Zanzibar, Dk. Masoud Rashid Mohamed, alisema ili kukabiliana na ushindani katika soko la ndani na nje, ni vema wakulima hao kuendelea kuzalisha kwa kiwango cha ubora zaidi.

Aliwasihi wakulima wasivunjike moyo na kuendelea kulima kwa juhudi na kuzingatia ubora wa bidhaa hizo ili kuendana na soko hilo.

Alisema serikali imekuwa ikithamini jitihada za wakulima hao na ndipo Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliona ni vyema kuwaongezea bei ya mwani baada ya kusikia kilio chao.

Aliwaahidi wakulima hao kuwa ujenzi wa kiwanda cha mwani kinachojengwa Chamanangwe kisiwani Pemba ukikamilika, wakulima watarajie bei zitabadilika na kuwa nzuri zaidi.

Mkurugenzi huyo, alisema zoezi la kuongeza bei za mwali litasaidia kuwakomboa wakulima hao kiuchumi na kuwataka kuzingatia uhifadhi wa mwani kwa matumizi ya binadamu na kulinda soko.


Greenlight Auction Mart

RIVERSIDE UBUNGO, DAR ES SALAAM - P.O. BOX 72260
TEL: +255 766 446 910
EMAIL: greenlightauctionmart@gmail.com

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**Greenlight Auction Mart Ltd, kwa kushirikiana na World Food Program (WFP), watakua na mnada mkubwa wa hadhara tarehe 27 Julai 2024, kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika katika maghala ya WFP yaliyopo Nala, Dodoma, takriban kilomita kumi kutoka katikati ya Dodoma. Bidhaa zitakazouzwa kwenye mnada ni pamoja na Mashine za Kusaga, Matrekta, Jenereta, vifaa mbalimbali vya Chuma na Alumini, na vipuri vya magari na jenereta, pamoja na mali nyingine zinazomilikiwa na WFP.**

1. ****Ukaguzi na Maelezo Zaidi****: Ukaguzi na maelezo zaidi kuhusu bidhaa zitakazouzwa zitatolewa katika maghala ya WFP yaliyopo Nala na Kizota, Dodoma, kuanzia Jumatatu, 15 Julai 2024, hadi Ijumaa, 26 Julai 2024, katika saa za ofisi (saa 3:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri). Bidhaa zote zitauzwa kama zilivyo (AS IS), na ni jukumu la mnunuzi kukagua na kununua bidhaa katika hali zao za sasa. Wala Greenlight Auction Mart Ltd wala WFP hawatawajibika kwa hali ya bidhaa hizo.

2. ****Ada ya Kuingia****: Wanunuzi wanapaswa kulipa ada ya kuingia, ambayo itarudishwa ndani ya siku tatu za kazi ikiwa hakuna bidhaa itakayonunuliwa. Muundo wa ada ni kama ifuatavyo:

- Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania (TZS 2,000,000/=) kwa wale wakaopenda kununua matrekta, forklifts, trela, mashine za kusaga, au jenereta kubwa.
- Shilingi Laki Mbili za Kitanzania (TZS 200,000/=) kwa watakaopenda kununua bidhaa zote nyingine.

Ada hii itawapatia washiriki nambari ya utambulisho kwa ajili ya mnada. Malipo ya ada ya kuingia yatasimamiwa na Greenlight Auction Mart Ltd kuanzia 15 Julai 2024 hadi 26 Julai 2024.

3. ****Masharti ya Malipo****: Washindi wa mnada wanapaswa kulipa kiasi kamili cha manunuzi siku ya mnada au ndani ya masaa 72 baada ya mnada. Ada ya kuingia inaweza kutumika kulipia bei ya manunuzi kwa ridhaa ya mnunuzi.

4. ****Kushindwa Kulipa****: Ikiwa mnunuzi atashindwa kulipa kiasi kamili ndani ya muda uliotajwa katika kifungu (3), au atajitoa kwenye malipo, ada ya kuingia itapokonywa na mauzo yatabatilishwa.

5. ****Kodi na Ushuru****: Ikiwa mnunuzi hana msamaha wa kodi, atapaswa alipe kodi zote zinazotakiwa na ushuru kwa bidhaa alizonunua ili kupata umiliki na kupokea hati za uhamisho. Baada ya malipo, mnunuzi atapokea nyaraka zinazohitajika kulipia kodi hizi na ushuru wa forodha. Wanunuzi watakuwa na siku tano (5) kukamilisha malipo haya. Kushindwa kufanya hivyo ndani ya kipindi hiki kutasababisha mnunuzi kuwajibika kwa gharama za uhifadhi.

6. **Kuondoa Bidhaa**: Bidhaa zilizonunuliwa ambazo hazihitaji malipo ya kodi au ushuru zinapaswa kuondolewa kwenye eneo la mnada ndani ya siku tano (5) za kazi kutoka tarehe ya mnada, baada ya malipo kamili na kupokea nyaraka zinazohitajika. Utoaji wa mashine za kusaga utaondolewa baada ya siku 15 kutoka tarehe ya mnada.

7. ****Bei ya Akiba****: Mauzo yote yatakuwa na bei ya akiba.

**Kwa taarifa Zaidi wasiliana nasi kwa Anuani: Greenlight Auction Mart Ltd:**
**RIVERSIDE UBUNGO, DAR ES SALAAM - P.O. BOX 72260**

**TEL : +255 766 446 910/0655 988 882/0763 949 437**
**EMAIL: greenlightauctionmart@gmail.com**
**Dar es Salaam, Jumatano Tairehe 10, Julai, 2024, Greenlight Auction Mart Ltd:**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## PASSPORT IMEPOTEA



**CLEMENTINA EPAFRAS ASSEY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASSPORT NO. **TAE725076** ILIYOTOLEWA 16/04/2024 DAR ES SALAAM. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU KUPITIA KUMBUKUMBU NAMBA: **PHQ/MWA/UKE/23794/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEOFREY ASSEY** ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA AKERI SECONDARY SCHOOL MWAKA 2009, CHENYE INDEX NO **S0986/0138.** ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA POLISI. TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/24612/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDWARD M MANWALI** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2661/0046/2018** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia Lunguya secondary school. Mwaka 2018 kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi .POLISI TAARIFA; **PHQ/MWA/MAG/2336/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUHIDINI MOHAMEDI MPINGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 370 DFK.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/141592/2024**

---

**Summons to appear (O.V.R.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**EXECUTION NO. 4002 OF 2024**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF ARCHIDIOCESE OF DAR ES SALAAM & ANOTHER.................D/HOLDERS**

**VERSUS**

**GIDEON JOHN MWIKOLA & OTHERS...............J/DEBTORS**

**TO: 1. ELIKA ELIA MASINGA**
**2. OLE A. LAIZER**
**3. SAID S. MKALONGEI**
**4. JUMAPILI SALUM WEBI**

**WHEREAS:** The above-named **DECREE HOLDER** has instituted the **APPLICATION FOR EXECUTION** against you, you are hereby summoned to appear in this court in persons or by advocate or agent duly authorized on 22nd day of JULY 2024 at 11:00 AM before **Hon. N. MWAKATOBE, DR** when a Judgement in respect of the filed suit will be delivered.
**TAKEN NOTICE** that, in default of your appearance the said Judgment will be delivered in your absence.
**GIVEN UNDER MY HAND** and the seal of the Court, this 4th day of JULY, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 234 YA MWAKA 2022**

**SYLVESTER YOHANA MTUMILA (Msimamizi wa mirathi ya Marehemu Yohana Chigwiye Mtumila ....................................... MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**EMMANUEL KUSAGA NA WENZAKE 2...... MJIBU MAOMBI**

**KWA: EMMANUEL KUSAGA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 16.08.2024 saa 3:00 asubuhi.
ANGALIZO: Kama hautahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 12 ya mwezi wa Julai, 2024.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA DODOMA**

**SHAURI LA MADAI NA. 9079/2024**

**FARAJA JOACHIM KIHONGOLE...........MDAI**
**DHIDI YA**
**PROJESTUS E. RWEGARULILA............MDAIWA**

**KWA: PROJESTUS E. RWEGARULILA**
**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA RUFAA NA. 9079/2024 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu Tanzania, Kanda ya Dodoma, mbele ya **Mhe. Jaji I. D. Musokwa,** wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (9:00) kamili asubuhi siku ya Jumanne tarehe 06/8/2024.
**HIVYO BASI;** unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO;** hautafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 Mwezi wa Julai, 2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 12852 OF 2024**

**In the matter of the estate of the late**
**JERALDINE DEODATUS JORDAN**

**And**

**In the matter of Application for Letters of Administration by**
**THOMAS ELIAMANI MMBANDO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 19 day of JULY 2024
Dated at DAR ES SALAAM this 19 day of JUNE 2024

Senior Resident Magistrate

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

HABARI KIMATAIFA

# Kagame atabiriwa ushindi Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

WACHAMBUZI wa masuala ya kisiasa nchini Rwanda wametabiri ushindi wa Rais Paul Kagame kutokana na ushawishi na sera zake zinazoonyesha kuwavutia Wanyarwanda wengi, pamoja na kuzuiwa kugombea wapinzani waliokuwa washindani wake wakubwa.

Hayo yalijiri wakati Rwanda ikiendelea na zoezi la upigaji kura jana kwa ajili ya kuwachagua rais na wabunge, ikielezwa kuwa kwa mara ya kwanza muhula wa urais utakuwa wa miaka mitano pekee, kutokana na mageuzi yaliyopitishwa mwaka 2015, ambayo pia yanamruhusu Rais Paul Kagame kuwania muhula wa nne.

Wakosoaji wa Rais Kagame wanasema kiongozi huyo anatarajiwa kushinda kwa urahisi katika kinyang'anyiro hicho kwasababu alizima upinzani.

Wengine walisema kuwa ni kutokana na namna alivyoendesha taifa hilo kuelekea kwenye amani tangu mauaji ya kimbari ya 1994, pale ambako takriban watu 800,000 wengi wakiwa wa Tutsi na wa Hutu waliuawa.

**Kipaumbele cha kwanza ni kupiga hatua iwezekanavyo kuelelekea kwenye usalama na uthabiti wa nchi yetu, maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kukuza taifa letu kuelekea ustawi.**

**SAFARI YA KISIASA**

Rais Kagame amekuwa madarakani nchini Rwanda kwa miaka 24 na ameiongoza nchi hiyo tangu kumalizika kwa mauaji ya kimbari ya Watutsi mwaka 1994.

Ilielezwa kuwa uchaguzi huo unafanyika wakati wapinzani wengine, ambao ni wakosoaji wakubwa wa Rais Kagame, wakitengwa kabisa kwenye kinyang'anyiro cha urais katika miezi ya hivi karibuni.

Miongoni mwao ni Diane Rwigara ambaye tayari alikuwa amezuiwa kugombea katika uchaguzi wa urais wa 2017, kwa kughushi waraka mwaka 2017. Na kwamba tume ya uchaguzi ilikataa tena kugombea kwake kwa madai kuwa hakuwasilisha dondoo za rekodi ya uhalifu, wala hati inayothibitisha uraia wake wa Rwanda.

Kuhusu mpinzani Victoire Ingabire, aliyehukumiwa mwaka 2013 kwa kula njama kupitia ugaidi na kupuuzia mauaji ya kimbari ya 1994, mahakama ilikataa ombi lake la kufanyia marekebisho ya haki zake za kiraia, ambazo zingemruhusu kukabiliana na Paul Kagame katika uchaguzi wa urais.

Ilielezwa kuwa wanawake hao wawili hawatarajii mengi kutokana na uchaguzi ambao wanaona umeamua mapema kuhusu Rais Kagame, licha ya kuelezwa kuwa kiongozi huyo hajawahi kupata chini ya asilimia 93 ya kura katika uchaguzi aliowahi kushiriki nchini humo.

Licha ya mafanikio yake ya kisiasa ndani na nje ya Rwanda kiongozi huyo pia anakabiliana na wapinzani wawili ambao wamedai kuwa amesalia madarakani kwa muda mrefu zaidi. Huku akisema kuwa wafuasi wake wanataka awanie kwa muhula mwingine.

Akizungumza baada ya kukamilisha mkutano wake wa mwisho wa kampeni, Kagame alisema kuwa vipaumbele vyake kwenye taifa ambalo amekuwa akiongoza tangu 2000 havijabadilika.

"Kipaumbele cha kwanza ni kupiga hatua iwezekanavyo kuelelekea kwenye usalama na uthabiti wa nchi yetu, maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kukuza taifa letu kuelekea ustawi," alisema Kagame.

Ilielezwa kuwa kiongozi huyo anachuana na wagombea wengine wawili akiwemo Frank Habineza wa Chama cha 'Democratic Green' aliyeshindana naye mwaka 2017, ambaye anasema anadai kuwa Kagame amesalia madarakani kwa muda mrefu zaidi.

Habineza aliiambia VOA kuwa amefanya kampeni kikamilifu kwenye karibu wilaya 30 kote nchini humo, na kwamba wapiga kura wakati huu wana imani kubwa naye.

"Nawapa matumaini kwamba baada ya miaka 30, tunahitaji kuona mambo kwa utofauti ikiwemo mtazamo, programu za kisiasa, mawazo na maoni tofauti. Hatutaharibu mema ambayo yamefanywa awali, lakini tunataka kuwapa matumaini mema, na kesho bora zaidi," alisema.

Kagame wakati akizungumza na wanahabari alisema kuwa hakutaka kuwa rais lakini chama chake kilisisitiza kuwa aingie kwenye kinyang'anyiro cha mwaka 2000. Miongo kadhaa baadaye, wafuasi wake wanamuomba aendelee kuwania.

"Kila siku naulizwa unaondoka lini? Hawa watu walionifanya rais wanasisitiza kuwa wanataka niendelee kuwa rais. Mtu mwingine anasema hapana, umedumu sana. Mimi huchanganyikiwa. Nafikiri siyo haki," alisema. **RFI, VOA**

## Biden awasihi Wamarekani kutuliza joto la kisiasa

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, ametoa wito kwa wananchi wake kutuliza joto la kisiasa baada ya jaribio la kumuua mpinzani wake katika uchaguzi ujao Donald Trump huko Pennsylvania.

Akizungumza jana kupitia ofisi ya Oval kwenye ikulu ya White House, mfumo ambao hutumika kwa rais wa Marekani kulihutubia taifa wakati wa mzozo tu, Biden alisema tofauti za kisiasa zisiwafanye kuwa maadui.

Kiongozi huyo pia aliwakumbusha raia wa nchi hiyo kwamba Wamarekani husuluhisha tofauti zao kupitia kura tu na wala sio mtutu wa bunduki.

Biden kwa mara nyengine alilaani tukio hilo dhidi ya Trump ambaye alipigwa risasi iliyokata sehemu ya sikio lake na kusababisha kuvuja damu. Ofisa mmoja wa zima moto aliyekuwa katika mkutano huo wa kampeni ya Trump alifariki dunia na watu wengine wawili kujeruhiwa vibaya.

Ilielezwa kuwa siku moja baada ya kuepuka jaribio hilo, Trump aliwasili Milwaukee huko Marekani ambako atateuliwa rasmi kama mgombea wa urais wa chama cha Republican baadae wiki hii.

Jaribio hilo la mauaji limezidisha machungu yaliyopo baina ya pande zinazohasimiana kisiasa Marekani. Huku Trump na Rais Biden wote wakitoa wito wa utulivu. **DW**



Wananchi wa Mukuru, Kitongoji cha Nairobi, wakiopoa miili ya watu waliokatwakatwa na kufungwa kwenye nailoni na kutupwa juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Polisi yamkamata mshukiwa mauaji Kenya

**NAIROBI,** Kenya

POLISI nchini Kenya wamesema wamemkamata mtu anayeshukiwa kuhusika na mauaji ya watu tisa ambao miili yao ilipatikana ikiwa imetupwa katika eneo la taka jijini Nairobi.

Kwa mujibu wa mkuu wa idara ya upelelezi nchini Kenya (DCI), Mohamed Amin, mshukiwa huyo alikamatwa jana katika mtaa wa Kayole Nairobi.

Aidha, DCI ilisema kuwa wamemuweka kizuizini mshukiwa mwengine katika tukio hilo la mauaji akiwa na simu ya mmoja wa waathiriwa.

Kaimu Inspekta Jenerali wa polisi nchini Kenya Douglas Kanja, alisema mshukiwa huyo mwenye umri wa miaka 33 alikamatwa katika oparesheni ambayo imefanywa na maofisa wake na wengine kutoka idara ya upelelezi.

Hata hivyo, polisi walisema kuwa uchunguzi unatarajiwa kufanyika kwa miili ya watu tisa ambayo imepatikana kwenye eneo la kutupa taka.

Tangu Ijumaa ya wiki iliopita miili iliyokatwakatwa vipande na kufungwa kwenye mifuko ya plastiki na magunia imetolewa kutoka kwenye lundo la takataka katika eneo la makazi duni la Mukuru kusini mwa mji mkuu, hali ambayo imezua wasiwasi.

Vile vile, juzi polisi walithibitisha kupata miili ya watu wanane, wote wakiwa ni wanawake. **RFI**

# GAMONDI AJIFUNGIA KUISOMA VITAL'O KUELEKEA MECHI CAF

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amesema siku mbili tatu zijazo ataanza kazi ya kuichunguza timu ya Vital'O ya Burundi ambayo watacheza nayo katika mechi ya awali, Ligi ya Mabingwa Afrika mwezi ujao.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, Kocha huyo alisema kwa sasa hajui chochote kuhusu timu hiyo, huku akiwa ameshafika Burundi mara moja tu, lakini anahitaji kuifahamu vizuri timu hiyo kwa kila kitu ili iwe rahisi kwake kuweza kukisuka kikosi chake kukabiliana nayo.**

Yanga imepangwa kucheza dhidi ya Vital'O, Agosti 16 mpaka 18, ambapo itakuwa ugenini jijini Bujumbura, kabla ya mechi ya marudiano nchini, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Agosti 23 hadi 25, mwaka huu.

"Kwa sasa sijui lolote kuhusu timu tunayocheza nayo, lakini kazi hiyo itaanza mara moja, nitaanza uchunguzi kuhusu kikosi chao, wako vipi, wanacheza vipi, wachezaji wao wana uwezo gani, kinanani ambao ni hatari na hata kuhusu nchi yao.

Siifahamu sana Burundi, nimeshawahi kufika mara moja, nadhani timu yao ya taifa ilikuwa inacheza dhidi ya Burkina Faso, Bujumbura si mbali sana na hapa, nadhani itakuwa faida kubwa kwa Yanga, kwani imeshatokea msimu uliopita tulipocheza dhidi ya El Merrikh ya Sudan nchini Rwanda, mashabiki walitupa sapoti kubwa, ilikuwa siku ya kukumbukwa," alisema kocha huyo.

Wakati Gamondi akisema hayo, zipo taarifa kuwa huenda mechi hiyo isichezwe Burundi, kwani mpaka sasa hakuna uwanja uliyoidhinishwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kwa ajili ya michezo ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Aliwataka wachezaji wa timu hiyo kucheza kwa ajili ya mashabiki, hasa wa Yanga ambao wamekuwa na mchango mkubwa sana kwenye mafanikio yao kwa miaka ya hivi karibuni.

"Lazima tuwatendee haki mashabiki wetu, wamekuwa wakijitoa sana, wakisafiri sehemu mbalimbali, wakati mwingine hadi nje ya nchi kutufuata, anatoa nauli zao, wanakata tiketi, wanatenga muda kwa ajili yetu, kusema kweli wao ni bora, hivyo ni lazima tuwape furaha ambayo ndiyo wanaipigania," alisema.

Kocha huyo alifichua kuwa aliamua kubaki Yanga kwa sababu moja ya kushindana kwenye michezo ya kimataifa ili kulipaisha soka la Tanzania.

"Nilibaki hapa si kwa sababu sikuwa na pa kwenda, ila niliamua kwa sababu ya kushindana kwenye michuano ya kimataifa nikiwa na Yanga, ili kutangaza na kuliheshimisha soka la Tanzania, wamenipokea vizuri na nimekuta mashabiki wake wanapenda sana soka," alisema kocha huyo.

Kikosi cha Yanga kwa sasa kipo Kigamboni kikijifua kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano na kabla hata ya kucheza mechi yao kwenye tamasha la Wiki ya Mwananchi, kinatarajia kwenda nchini Afrika Kusini kucheza mchezo wa Kombe la Toyota, dhidi ya Kaizer Chiefs, ambayo msimu uliopita iliialika kwenye tamasha lao lililochezwa, Julai 22, mwaka jana na kushinda bao 1-0 lililowekwa wavuni na Kennedy Musonda.

## RAHA KWELI...




Nahodha na mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, akinyanyua kombe juu huku akisherehekea na wachezaji wenzake baada ya kutwaa ubingwa wa Copa America kwa kuifunga Colombia bao 1-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa jana katika Uwanja wa Hard Rock, Miami nchini Marekani. **HABARI UK. 22.** **PICHA: MTANDAO**

# *Samia/Katambi Cup yazinduliwa Shinyanga*

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

LIGI ya Samia/Katambi Cup ya mpira wa miguu, imezinduliwa jana katika viwanja vya Jasco vilivyopo Ngokolo, Shinyanga huku ikishereheshwa kwa michezo mbalimbali ikiwamo kuvuta kamba, kukimbiza kuku na kuchoma nyama, ambapo washindi waliibuka na zawadi.

Jumla ya timu 32 za mpira wa miguu zitatimua vumbi katika viwanja mbalimbali kwenye ligi hiyo ambayo imelenga kuibua vipaji vya vijana.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ligi hiyo, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, alimpongeza Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi kwa kuona umuhimu wa kuibua vipaji vya vijana kwa kuwa soka sasa ni ajira.

"Rais Samia Suluhu Hassan anapenda michezo, hivyo Katambi kuanzisha ligi hii ni kumuunga mkono katika kukuza michezo hapa nchini na kutoa ajira kwa vijana," alisema Mwinjuma.

Aidha, alitaja zawadi ambazo watapewa washindi kwenye ligi hiyo; mshindi wa kwanza wa mpira wa miguu atapewa Sh. milioni sita pamoja na kombe, mpira na jezi, mshindi wa pili atapewa Sh. milioni tatu, kombe, mpira na jezi, huku mshindi wa tatu yeye akiiondoka na Sh. milioni moja, mpira na jezi.

Mfungaji bora alisema atapewa Sh. 50,000, mchezaji mwenye nidhamu Sh.100,000 na washindi wa kucheza wa kwanza atapewa Sh. milioni moja, wa pili Sh. 500,000 na watatu Sh. 300,000.

Kwa upande wa Katambi ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, alisema lengo la ligi hiyo ni kuibua vipaji vya vijana, ambao watapata ajira kwenye timu mbalimbali ikiwamo Stand United ambayo wapo kwenye mikakati ya kuipandisha kushiriki kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

# Ngara Ruhoro Marathon sasa rasmi Julai 27

**Na Judith Julius, Ngara**

MBIO za nusu marathon zijulikanazo kama Ngara Ruhoro Marathon zinatarajiwa kufanyika wilayani Ngara mkoani Kagera Julai 27, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Ofisa Utamaduni, Sanaa na Michezo Wilaya ya Ngara Said Salum, mbio hizo zinaratibiwa na ofisi yake na kudhaminiwa na Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ndaisaba George Ruhoro.

Salum alisema mbio hizo zitakazoshirikisha wakimbiaji wa kike na kiume, zinalenga kujenga umoja, mshikamano, na uhusiano.

Alisema mbio hizo vile vile zinalenga kuhamasisha wananchi wa wilaya hiyo kushiriki katika michezo, kuibua, na kukuza wanariadha.

Salum aliongeza kuwa mbio hizo zitashuhudia washiriki wakikimbia umbali wa kilometa tano, 10, na 21.

Alisema mbio hizo hufanyika kila mwaka, wakati ambapo hakuna mvua, ili kuepuka utelezi na tope vinavyoweza kuwaathiri wanariadha.

Kwa mujibu wa afisa huyo, waandaaji waliamua kuandaa mbio hizo katika kipindi hiki kwani hakuna shughuli zinazoweza kuwaletea vizuizi washiriki mbio hizo.

Salum alibainisha kuwa Ruhoro ameandaa zawadi kadhaa zitakazotolewa kwa washindi wa mbio zote tatu, ambapo mshindi wa kwanza hadi wa tatu kwa kila mbio atapewa fedha taslim.

Alisema kundi la pili, ambalo ni la wanamichezo wote watakaoshiriki, litapewa motisha ili lishiriki katika mbio hizo msimu ujao.

Ofisa huyo alisema wananchi wote wilayani humo wanakaribishwa kushiriki katika mbio hizo kwani ushiriki wao utawapa ukakamavu na kuwaepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Mbio hizo zitashirikisha wanamichezo waliomo ndani ya Wilaya ya Ngara na zitaanzia Uwanja wa Posta ya Zamani kwenda barabara kuu iendayo nchini Burundi.

Salum alisema Chama cha Riadha cha Wilaya ya Ngara (CHANINGA), kitashirikiana na ofisi yake kuratibu mbio hizo.

Alisema Ngara Ruhoro Marathon imekuwa chachu kwa wananchi wengi kushiriki katika mchezo huo kwani inawakutanisha na mwakilishi wao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## ZISIKUPITE

### ZIRKZEE RASMI ATUA UNITED

KLABU ya Manchester United imemsajili mshambuliaji wa Bologna na Uholanzi, Joshua Zirkzee, kwa mkataba wenye thamani ya pauni milioni 36.5, Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ametia saini mkataba wa miaka mitano Old Trafford, na chaguo la kuuongeza kwa miezi 12 zaidi. ***(Mail)***

### GUEHI ASAKWA LIVERPOOL

MARC Guehi anasakwa na Liverpool, ambao wameanza mazungumzo ya kumsajili beki huyo wa kati wa Crystal Palace na England mwenye umri wa miaka 24. ***(Fabrizio Romano)***

### SETFORD SAFI ARSENAL

ARSENAL imefikia makubaliano ya kumsajili mlinda mlango wa Kimataifa wa England, Tommy Setford (18), kutoka Ajax. ***(Athletic)***

### WHARTON AKATAA OFA

KIUNGO wa kati wa England, Adam Wharton mwenye umri wa miaka 20, amekataa ofa kutoka Manchester City, Bayern Munich na Real Madrid ili kusalia Crystal Palace. ***(Sun)***

### MERINO AWANIWA ARSENAL

ARSENAL inapigiwa upatu kuishinda Aston Villa katika harakati za kumnunua kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Mikel Merino mwenye umri wa miaka 28, msimu huu. ***(Mundo Deportivo)***

### AHMEDHODZIC AWANIWA

KLABU ya Wolves inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumnunua mlinzi wa Sheffield United mwenye thamani ya pauni milioni 20, Anel Ahmedhodzic mwenye umri wa miaka 25, kuchukua nafasi ya Muingereza Max Kilman (27), aliyejiunga na West Ham. ***(Sun)***

### ALVAREZ ATAKIWA PSG

KLABU ya Manchester City itafanya mazungumzo na mchezaji wao wa Kimataifa wa Argentina, Julian Alvarez mwenye umri wa miaka 24, baada ya Copa America. Paris St-Germain wanavutiwa na mshambuliaji huyo, ambaye anataka muda zaidi wa kucheza, lakini City wanataka kusalia naye. ***(Fabrizio Romano)***

### TERLAND AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United iko tayari kumsajili mshambuliaji wa Norway, Elisabeth Terland, kutoka Brighton mwenye umri wa miaka 23. ***(Guardian)***

### JAKUB KURUHUSIWA GUNNERS

MCHEZAJI Jakub Kiwior ataruhusiwa kuondoka Arsenal msimu huu wa majira ya joto na beki huyo wa Poland mwenye umri wa miaka 24, anavutiwa na klabu za Serie A. ***(Football Insider)***

### INACIO ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wamemweka mlinzi wa kati wa Sporting Lisbon na Ureno, Goncalo Inacio mwenye 22, kuwa mlengwa wao mkuu katika kipindi hiki cha uhamisho. ***(CaughtOffside)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# YAMAL AVUNJA REKODI YA PELE HISPANIA IKIBEBA EURO

**BERLIN,** Ujerumani

## Ni ile ya Kombe la Dunia iliyodumu tangu 1958, mwenyewe asema ni ndoto na...

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Lamine Yamal, amekuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kushiriki katika fainali ya Kombe la Dunia la FIFA au Kombe la Mataifa ya Ulaya (Euro), Jumapili dhidi ya England, na kuipita rekodi iliyowekwa na gwiji wa Brazil Pele mwaka 1958.

**Jumamosi Yamal alifikisha umri wa miaka 17 na mchezaji huyo wa Barcelona alisherehekea kwa kusaidia bao la kwanza na kuliwezesha taifa lake kuishinda England mabao 2-1 na Hispania ikibeba ubingwa wa Euro kwa mara ya nne nchini Ujerumani juzi.**

Alitwaa tuzo ya Mchezaji bora chipukizi wa mashindano hayo.

"Ni ndoto na siwezi kusubiri kurejea Hispania kusherehekea," alisema Yamal akiiambia TVE.

"Ni zawadi bora zaidi ya siku ya kuzaliwa ambayo ningeweza kupokea. Sasa nataka kwenda kusherehekea na familia yangu.

"Baada ya wao kusawazisha, walikandamiza sana. Lakini sijui timu hii inaundwa na nini, lakini huwa tunaishia kurejea."

Yamal alimaliza michuano hiyo akiwa na bao moja na asisti nne, pasi nyingi zaidi katika michuano ya Ulaya tangu rekodi zilipoanza kutunzwa mwaka 1980.

Pia akawa mchezaji wa kwanza kufunga au kusaidia upatikanaji wa bao katika robo fainali, nusu fainali na fainali ya Euro moja.

Pele, aliyefariki mwaka 2022, alikuwa na umri wa miaka 17 na siku 249 alipoichezea Brazil fainali ya Kombe la Dunia 1958, akifunga mara mbili katika ushindi wa 5-2 dhidi ya Sweden. Ni mara ya pili ndani ya wiki Yamal kuvuka alama iliyowekwa na Pele. Katika ushindi wa katikati ya juma dhidi ya Ufaransa, alikuwa mchezaji mchanga zaidi kushiriki nusu fainali ya mashindano makubwa ya timu ya taifa.

"Pele Foundation inampongeza Lamine Yamal kwa hatua hii muhimu katika kazi yake na inatamani kwamba hii ni hatua ya kwanza ya safari ndefu na ya ushindi," ilisema taatifa ya mfuko wa hisani wa Pele.

Imekuwa mashindano ya rekodi kwa Yamal.

Akawa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kucheza kwenye michuano ya Euro katika mechi ya ufunguzi ya Hispania dhidi ya Croatia na kisha mfungaji mwenye umri mdogo zaidi katika fainali hizo alipofunga katika ushindi wa nusu fainali dhidi ya Ufaransa.

"Tumeona fikra, zao la fikra," alisema kocha wa Hispania, De la Fuente katika mkutano na wanahabari baada ya mechi hiyo.

Yamal amekuwa Barca tangu akiwa na umri wa miaka saba na alicheza kwa mara ya kwanza katika timu ya wakubwa mwaka jana akiwa bado na umri wa miaka 15.

Msimu uliopita, akiwa na umri wa miaka 16, alicheza mechi 50 katika mashindano yote kwa klabu yake, akifunga mabao saba na kusaidia 10.

HABARI MICHEZO

# MESSI ABEBA COPA AMERICA YA PILI KWA MACHOZI



**MIAMI,** Marekani

LIONEL Messi alilazimika kutoka nje baada ya kupata jeraha la kifundo cha mguu wa kulia katika kipindi cha pili cha ushindi wa bao 1-0 wa Argentina katika fainali ya Copa America dhidi ya Colombia kwenye Uwanja wa Hard Rock, Miami, Jumapili hapa Marekani.

Lautaro Martinez aliifungia Argentina bao hilo la ushindi katika muda wa nyongeza na kuipa Argentina taji lao la 16 la Copa America na taji la tatu mfululizo la michuano mikubwa baada ya kushinda taji hilo mwaka 2021 na Kombe la Dunia 2022.

Messi alianguka uwanjani katika dakika ya 64 na mara moja alionesha wasiwasi wake kwa benchi la Argentina. Alibaki chini kwa dakika kadhaa huku wakufunzi wakitoka kabla ya kumsaidia kusimama na kuvua kiatu chake kwenye mguu wake wa kulia.

Alipotoka nje ya uwanja, mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or mara nane alivua kitambaa chake cha unahodha na kutupa kiatu chake chini kwa kufadhaika.

Messi mwenye hisia kali wakati huo alioneshwa akifunika uso wake, akilia kwenye kiti chake, huku kamera za televisheni zikionesha pia kifundo cha mguu wake wa kulia kilikuwa kimevimba sana.

Nafasi yake ilichukuliwa na Nicolas Gonzalez. Messi alikuwa ameshuka chini akishikilia kifundo cha mguu wake wa kulia baada ya changamoto kali katika kipindi cha kwanza.

Mchezaji huyo wa Klabu ya Inter Miami, aliufukuzia mpira na kujaribu kuupiga kabla haujatoka nje ya mipaka. Aliuweka mguu wake wa kulia kwa shida na alionekana kupata mawasiliano kutoka kwa Santiago Arias wa Colombia.

Messi alikuwa akiuguza jeraha la mguu na kukosa raha katika sehemu kubwa ya michuano hiyo na alikosa mchujo wa hatua ya makundi ya Argentina. Alipata jaribio moja la kufunga katika kipindi cha kwanza Jumapili katika mechi hiyo timu hizo zikiwa suluhu kabla yajatoka.

"Leo ndiye mchezaji mkubwa zaidi katika historia. Hataki kamwe kuondoka uwanjani. Ana kifundo cha mguu kilichovimba na anataka kuendelea kucheza," alisema Kocha wa Argentina, Lionel Scaloni baada ya mchezo huo.

"Napendelea wachezaji hao na wachezaji wenzake waone hivyo, kwamba ana umri wa miaka 30 na yupo na anataka kuchangia, anataka kucheza sio kwa sababu ya kujikweza au ubinafsi.

"Anataka kuendelea kucheza kwa sababu hataki kuwaacha wenzake, hataki kuwaacha uwanjani hata akiwa katika hali hiyo... hajisikii vizuri inapobidi kuondoka na yeye, alizaliwa kuwa uwanjani."

## Southgate kuamua mustakabali wake England

**BERLIN,** Ujerumani

GARETH Southgate amesema uamuzi juu ya mustakabali wake wa kuendelea kuinoa England si "kwa sasa" na atazungumza na "watu muhimu nyuma ya pazia" siku zijazo baada ya kushindwa kwenye fainali ya Euro 2024 na Hispania Jumapili.

'Simba Watatu' hao wamekuwa timu ya kwanza kupoteza fainali mbili mfululizo za Euro huku Mikel Oyarzabal akifunga bao la ushindi dakika ya 86 na kuipa Hispania ushindi uliostahili wa mabao 2-1 mjini Berlin.

Nico Williams hapo awali aliipatia Hispania bao la kuongoza dakika ya 47 kabla ya Cole Palmer aliyetokea benchi kusawazisha dakika 17 kabla ya mchezo kumalizika.

Mkataba wa sasa wa Southgate unamalizika Desemba na vyanzo vimeiambia ESPN kwamba FA inataka kocha huyo mwenye umri wa miaka 53, abaki kwenye wadhifa hadi Kombe la Dunia la 2026 akiwa amefika fainali mbili, nusu fainali na robo fainali wakati wa mashindano yake manne.

Hata hivyo, Southgate amekabiliwa na shutuma za hadharani wakati wa fainali hizi kwa mtazamo wake wa kihafidhina na aliliambia gazeti la Ujerumani Bild kabla ya mchuano huo kwamba kama England haitanyanyua taji lao la kwanza la wanaume katika kipindi cha miaka 58, "pengine sitakuwa hapa."

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wake, Southgate aliiambia ITV: "Sidhani sasa ni wakati mzuri wa kufanya uamuzi kama huo. Ninahitaji kuzungumza na watu sahihi. Sio kwa sasa."



## *Muller atundika daluga Ujerumani*

**BERLIN,** Ujerumani

THOMAS Muller amethibitisha kustaafu kuichezea Ujerumani baada ya michuano ya Euro 2024, na kuhitimisha soka lake la kimataifa akiwa na mechi 131 na mabao 45.

Mshambuliaji huyo wa Bayern Munich ni wa tatu kwa wachezaji walioichezea mechi nyingi zaidi Ujerumani, akiwa nyuma ya Miroslav Klose (137) na Lothar Matthäus (150).

"Siku zote nilikuwa najivunia kuwakilisha nchi yangu. Ninataka kuwashukuru nyote," alisema Muller kwenye video ya YouTube akitangaza uamuzi wake.

"Sasa mimi ni shabiki kwenye jukwaa."

Muller alicheza mechi yake ya kwanza katika timu ya taifa katika mechi ya kirafiki dhidi ya Argentina mwaka 2010 na aliibuka kuwa maarufu wakati wa Kombe la Dunia la mwaka huo, akifunga mabao matano na kutoa pasi tatu za mabao na kumaliza kama mshindi wa Kiatu cha Dhahabu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alianza vema Kombe la Dunia 2014, akifunga hat-trick katika mchezo wa ufunguzi wa makundi wa Ujerumani dhidi ya Ureno.

Alianza mechi zote saba za Ujerumani kwenye michuano hiyo, akifunga katika mechi tatu ikiwamo ile maarufu ya kubomolewa 7-1 Brazil kwenye nusu fainali.

Muller alicheza dakika zote 120 za fainali dhidi ya Argentina huku timu ya Joachim Low ikishinda 1-0 na kushinda Kombe la Dunia.

Uamuzi wa Muller unamaanisha kuwa Kocha wa Ujerumani, Julian Nagelsmann, atakosa kiungo mwingine wa muda mrefu wa timu ya taifa baada ya Toni Kroos kustaafu soka.

Mustakabali wa kimataifa wa mlinda mlango Manuel Neuer pia uko shakani. Neuer mwenye umri wa miaka 38, ni mchezaji wa tano wa Ujerumani aliyecheza mechi nyingi zaidi akiwa nazo 124.

# HABARI MICHEZO

## Kuelekea Olimpiki Paris

INATOKA UK. 24

Aliendelea kufafanua, "TOC na IOC inaheshimu utumiaji wa viatu vya mashindano (spikes/ marathon race shoes) kwa wanamichezo wenye mikataba yao binafsi, lakini siyo training shoes na mavazi wakati wa michezo ya Olimpiki.

"Vyama vya michezo vina Mashindano yao Kimataifa, (Kanda, Bara na Dunia), ambavyo wanaweza kusaini mikataba kwa ajili ya mashindano hayo tu, si Olimpiki na Jumuiya ya Madola. Natoa rai kwa vyama vya michezo, wanaposaini mikataba na makampuni ya vifaa vya michezo wasihusishe michezo ya Jumuiya ya Madola na Olimpiki.

Alipoulizwa kuhusu kambi ya pamoja ya wawakilishi wote wa Olimpiki 2024, Bayi akajibu; "TOC haitakuwa na kambi kama ilivyozoeleka, kwani wachezaji wote waliofikia viwango vya Paris 2024 wa Riadha wawili wa kiume (Simbu na Geay) walikuwa kwenye udhamini mzito wa Olympic Solidarity.

"Wanariadha wa kike wawili (Magdalena na Jackline) waliofikia viwango vya kushiriki Paris 2024 watakuwa na udhamini wa TOC mpaka Julai 30, 2024.

Kuhusu wachezaji wengine; (Mlugu anayecheza judo) na (Collins - kuogelea), wao walikuwa kwenye udhamini wa Olympic Solidarity na World Aquatics, isipokuwa Sophia Latiff, ambaye licha ya kutofikia viwango, alipewa nafasi ya upendeleo (Universality)," anamaliza Bayi.

Alipotafutwa Kaimu Katibu Mkuu wa RT, Wakili Jackson Ndaweka, alikiri wazi kwamba uhalali wa kuvalisha wanamichezo wanaoshiriki Olimpiki ni wa TOC, lakini isingekuwa rahisi kwao kukataa udhamini wa Xtep, uliokuja miaka 16 tangu walipovunjiwa mkataba kwa mtindo huo huo mwaka 2008 kuelekea Olimpiki ya Beijing, China.

"Kwa nafasi yake (Bayi) kama Katibu wa TOC, aliwahi kutuandikia barua RT kuuliza juu ya uwapo wa mkataba baina yetu na Xtep, nilimjibu kwa maandishi kuwa ni kweli na nikaenda mbali zaidi kwa kumueleza moja ya matakwa ya kimkataba ni kutumia vifaa vyao katika Olimpiki.

"Pia nikamweleza kwamba kwa zaidi ya miaka 16 tangu TOC waliposababisha mkataba wetu na Kampuni ya Li Ning kuvunjika baada ya kuvalisha wanamichezo wetu vifaa vya Kampuni ya Puma, RT haikuwa na mdhamini wa vifaa, jambo ambalo limetupa wakati mgumu sisi kama shirikisho na Serikali, ambao tulilazimika kununua vifaa.

"Kupitia barua yangu hiyo kwake, nikaiomba TOC ituruhusu wanariadha wetu wavae vifaa vya Xtep, ili si tu kumlinda mdhamini wetu ambaye ataendelea kutupa vifaa hata baada ya Olimpiki, bali kutopoteza bonasi kubwa zilizoko mezani kwa wanariadha wetu iwapo watarudi na medali katika Olimpiki 2024.

"Xtep wameweka mezani Dola 50,000 kwa mwanariadha atakayetwaa medali ya Dhahabu, Dola 30,000 kwa medali ya Fedha na Dola 20,000 kwa medali ya Shaba, hizi ni bonasi ambazo hata ukiwatafuta kina Simbu, Geay na wengineo, watakwambia wanavyopambana kupata pesa za ushindi na bonasi hizo.

"Sasa kama TOC watashikilia msimamo kwamba wanaraiadha wetu watavalishwa vifaa vya Asics na si Xtep, sisi kama shirikisho tutachukua hatua. Wanayo mamlaka ya kuwavalisha Assics, lakini sisi ili kuondoa hatari hiyo ya kuwavalisha vifaa vya mpinzani wa mdhamini wetu.

"Hatutaruhusu wala kukubali watuvunjie mkataba ambao una manufaa kwetu hata baada ya Olimpiki, tutapata sapoti gani kutoka kwao kupitia mdhamini wao baada ya Olimpiki? Wachezaji watanufaikaje na kutumia vifaa vya mdhamini wao baada ya mshindano? Hapa ndipo tunaposema tutachukua hatua," alisema.

**ALPHONCE SIMBU AFUNGUKA**

Kwa upande wake, Simbu alikiri kupata kizungumkuti, kwani anaamini unahusisha mamlaka ambazo zinapaswa kukaa kwenye meza ya mazungumzo ili kupata suluhu itakayowapa fursa ya wao kushindana wakiwa kwenye mavazi ya Xtep, kwani wana ari kubwa ya kutwaa dola za bonasi hizo

"Kimantiki RT ndio yenye wachezaji na mikataba mingi inasainiwa na RT, na kama Xtep ni mdhamini wa shirikisho, basi ni bora wakatuacha tukatumia vifaa vyao, ingawa pia natambua kwamba wenye mamlaka ya kutuvalisha ni kamati na sio shirikisho."

Naye Mjumbe wa Chama cha Riadha Mkoa wa Dar es Salaam (DAA), na Kocha wa siku nyingi, Kapteni Mstaafu Lucas Nkungu, alisema hatamani kuona tukio la 2008 likijirudia tena, kwani itakuwa pigo kwa mchezo wa riadha na kuomba serikali kupitia wizara yenye dhamana, kuingilia kati na kuhakikisha muafaka unapatikana.

# SIMBA YAJIVUNIA KUSAJILI KIKOSI CHA KIZAZI KIPYA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema idadi ya wachezaji wapya iliyowasajili msimu huu ni wengi zaidi kusajiliwa kwa mkupuo kwa miaka tisa iliyopita, ikisema ilichofanya ni mapinduzi ya kuanza upya, wakiwa na kikosi cha kizazi kipya.

Akizungumza kutoka Ismailia nchini Misri ambako wameweka kambi kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano, Mratibu wa timu hiyo, Abbas Ally, alisema hata yeye hajawahi kuona Simba ikisajili wachezaji wengi wapya kwa mkupuo mmoja, hivyo inaonyesha kuwa viongozi wa klabu hiyo, akiwamo Mwekezaji, Rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed 'Mo' Dewji, wamedhamiria kuijenga timu mpya kabisa.

"Usajili huu una maana kubwa sana katika kikosi cha Simba kwa sababu tangu 2015, hakujawahi kufanyika mabadiliko makubwa kwenye kikosi kama mwaka huu. Mimi niko hapa tangu 2015, sijawahi kuona kitu kama hiki, kwa hiyo haya ni mapinduzi na huu ni mwanzo mpya.

> **"Watu wanataka kuona Simba yao ile ambayo wameizoea, ile ambayo inamiliki sana mpira, inamiliki mchezo kwa kiasi kikubwa na kuwapa wakati mgumu wapinzani na iliyokuwa inafanya vizuri karibuni kila mchezo, ikiwamo kupata makombe karibuni yote yanayokuwa mbele yao," alisema Abbas.**

Alisema kwa miaka mitatu iliyopita wanachama na mashabiki wa klabu hiyo hawakuwa na furaha kutokana na kikosi chao kutokukuwa kwenye kiwango kisichoridhisha na kutopata matokeo, hivyo imewasukuma viongozi kufanya mabadiliko kama hayo.

Aliwatoa wasiwasi baadhi ya mashabiki ambao wanaona kuwapo kwa wachezaji wengi kutachelewesha muunganiko wa wachezaji.

"Unajua matokeo ya misimu mitatu imewavunja sana watu mioyo yao, tulijaribu kukijenga kikosi, lakini timu ilikuwa haichezi vizuri na matokeo hayakuwa mazuri, ndiyo maana wanahofu wingi wa wachezaji wengi waliosajiliwa kama wanaweza kuunganika kwa muda mfupi, wana haki, lakini nadhani tukiwa tunapata ushindi kwenye michezo yetu hayo yote watayasahau," alisema mratibu huyo.

Alisema haamini kama watachukua muda mrefu kutokana na umahiri wa benchi la ufundi lililopo na umri mdogo wa wachezaji ambao ni rahisi kushika maelekezo.

"Ukiangalia mchanganyiko wa wachezaji tulionao ni vijana, wana umri mdogo, ni wepesi kushika maelekezo, ni timu ya kizazi kipya, mimi naamini baada ya mwezi tu, aina ya benchi la ufundi tulilonalo na aina ya wachezaji tulionao, tupakuwa na kikosi bora sana na watu wataamini kuwa katika soka kila kitu kinawezekana hata kwa muda mfupi," alisema.

## RAHA YA UBINGWA...



Nahodha wa Timu ya Taifa ya Hispania, Alvaro Morata (aliyebeba kombe), akishangilia pamoja na wachezaji wenzake baada ya kuutwaa ubingwa wa Euro 2024 kwa kuifunga England mabao 2-1, kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Ujerumani juzi. Kushoto waliokumbatiana ni Nico Williams na Lamine Yamal wenye asili ya Afrika, ambao kwa kiasi kikubwa waliibeba timu yao mabegani mwao. **PICHA: MTANDAO**

# Serikali yapongeza VAR kutua nchini

INATOKA UK. 24

kigeni, ambapo kabla ya hapo zilikuwa hazifanyi vema.

"Kwa takwimu tulizonazo wachezaji wa kigeni hawajafika 70 kati ya wachezaji 600 ambao huwa wanashiriki Ligi Kuu, hivyo wachezaji wetu wanatakiwa na wao watoke nje ili wakapate changamoto na siyo sisi kupunguza idadi ya wachezaji wa kigeni," alisema Rais Karia.

Alisema wachezaji wa kigeni wameongeza ushindani kwenye Ligi Kuu na kuchangia kukua kwa viwango vya wachezaji wa ndani, kiasi cha kuisaidia timu ya taifa kufanya vizuri.

"Tulipokuwa tukicheza na DR Congo na Zambia, wachezaji wengi wa Tanzania walikuwa wa ligi ya ndani na wadogo, lakini walifanya vizuri sana kiasi cha kushangaza wengi, kwa sababu hawana tena ule woga wa kuogopa wachezaji wa kigeni, kila siku wanacheza na wachezaji hao hao kwenye ligi au wapo timu moja, hiyo imetusaidia sana kama taifa," alisema.

Michezo
Jumanne Julai 16, 2024
Nipashe



Messi abeba Copa America ya pili UKURASA 22

IMEWASILI...



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua gari la kisasa la kurushia matangazo (OB Van), baada ya kulizindua, kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam jana. Tukio hilo likitanguliwa na uzinduzi wa mfumo wa kumsaidia mwamuzi uwanjani (VAR). **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Kuelekea Olimpiki Paris 2024, TOC, RT zavutana

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Tanzania hatarini kufungiwa, msuguano wa udhamini wafurukuta, serikali...

WAKATI homa ya Michezo ya Olimpiki ya majira ya joto itakayoanza kutimua vumbi Julai 26 na kumalizika Agosti 11, mwaka huu, jijini Paris, Ufaransa likizidi kupanda, msuguano mkali umeibuka nchini baina ya Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) na Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), imefahamika.

**Kawaida TOC ndio mratibu wa ushiriki wa Tanzania katika michezo hiyo itakayofunguliwa na Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa, ambako Tanzania itawakilishwa na wanamichezo saba tu, kutoka katika michezo mitatu ya Riadha (wakimbiaji wanne), Judo (mchezaji mmoja) na Kuogelea (waogeleaji wawili).**

Katika riadha, Tanzania itawakilishwa na Alphonce Simbu na Gabriel Geay (marathon wanaume), Jackline Sakilu na Magdalena Shauri (marathon wanawake), judo itawakilishwa na Andrew Mlugu, huku Collins Saliboko na Sophia Latiff wao wakibeba bendera ya uogeleaji (wanaume na wanawake).

Tayari nyota hao wanaendelea na mazoezi yao ya mwisho yanayosimamiwa na vyama vya michezo yao au kwa udhamini wa TOC na Olympic Solidality (OS), lakini tayari msuguano umeibuka unaoitishia ari ya ushiriki ya baadhi yao, idadi yao na hata ustawi wa mafanikio yao na michezo kwa ujumla.

Kwa mujibu wa taarifa, RT mwaka jana lilisaini mkataba wa ufadhili na udhamini wa vifaa vya michezo na pesa za bonasi na Kampuni ya Xtep ya China, unaoitaka kampuni hiyo kuzivalisha timu zote za riadha zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa, pamoja na bonasi ya fedha kwa washindi.

Kupitia mkataba huo, Xtep mwaka jana ilitoa mafungu 50 ya vifaa vya michezo ikiwamo mavazi na viatu, ambako mwaka huu inaipa RT mafungu 250 ya vifaa hivyo, pamoja na bonasi ya Dola 50,000 kwa mshindi wa medali ya Dhahabu, Dola 30,000 medali ya Fedha na Dola 20,000 kwa medali ya Shaba.

Lakini zikiwa zimebaki wiki mbili kuelekea ufunguzi wa Olimpiki ya Paris, Katibu Mkuu wa TOC, Filbert Bayi, kupitia mahojiano maalum, ameweka wazi kwamba hawautambui mkataba huo na kwamba jukumu la kuwavalisha wachezaji wanaoshiriki Olimpiki na Michezo ya Jumuiya ya Madola ni la TOC, kupitia mdhamini wao, Asics.

Akizungumza na mwandishi wetu alipotaka kujua suala la RT kutumia udhamini wa Xtep, Bayi alisema, "kwa kifupi jibu la swali lako ni hawana nafasi kabisa. Michezo ya Olimpiki siyo ya Judo, Riadha na Kuogelea tu, kuna michezo zaidi ya 30 itakayoshiriki Paris 2024.

"Kwa mfano Tanzania iwe na wawakilishi wa michezo zaidi ya mitano, kwa hiyo kila mchezo uwe na udhamini wa vifaa vyake watakavyotumia katika Michezo ya Jumuiya ya Madola au Olimpiki, hiyo itakuwa timu ya Taifa au itakuwa vurugu? Alihoji na kuendelea;

"Katiba ya TOC na 'Olympic Charter,' mamlaka ya kupeleka na kuvalisha timu ya kushiriki Jumuiya ya Madola au Olimpiki ni ya Kamati za Olimpiki na si vinginevyo. Kabla ya vyama/mashirikisho ya michezo kuingia mikataba yao, nashauri wasome Katiba ya TOC na 'Olympic Charter.'"

INAENDELEA UKURASA 23

# Serikali yapongeza VAR kutua

**Shufaa Lyimo Adam Fungamwango**

SERIKALI imesema kupatikana VAR ambayo itatumika kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, kutapunguza malalamiko waliyokuwa wanatupiwa waamuzi kwa kile kilichokuwa kinaonekana hawafanyi maamuzi sahihi.

Akizungumza jana kwenye hafla ya uzinduzi wa video ya usaidizi wa waamuzi maarufu kama VAR, uliofanyika kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, alisema kuwapo kwa kifaa hicho kitawezesha waamuzi kufanya maamuzi yao sahihi kwani watakuwa na uwezo wa kurudia kile ambacho watakuwa hawajakiona, ili timu ziweze kupata ushindi wa halali.

Aidha, Waziri Majaliwa, alitaka viwanja ambavyo havina ubora, viwekwe pembeni kwani kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu, vitaharibu mvuto wa ligi yenyewe.

"Nampongeza Rais Karia (Wallace) kwa juhudi kubwa tangu aanze kulisimamia Shirikisho la Mpira wa Miguu tumepata mafanikio makubwa kupitia mpira wa miguu, na kwa maboresho haya naamini Tanzania itapanda na kushika nafasi ya nne kwenye Ligi ya Afrika kutokana na uwekezaji huu," alisema Waziri Mkuu.

Alisema serikali inalitaka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kuendelea kushirikiana na kampuni zilizowekeza kwenye utangazaji wa michezo mbalimbali nje na ndani ya nchi, ili kukuza soka la nchi na kulitangaza nje, pamoja na kuwaweka sokoni wachezaji wa Kitanzania.

Kabla ya kumkaribisha Waziri Mkuu, Rais wa TFF, Karia, alisema kuwa wameamua kubaki na idadi ya wachezaji 12 wa kigeni licha ya wadau wengi kutaka idadi hiyo ipunguzwe.

Alisema sababu kuwa ni kwamba klabu za Tanzania zimepata mafanikio makubwa kwa miaka ya hivi karibuni kutokana na kuwa na wachezaji wa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >